# Nipashe

Alhamisi Agosti 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580303

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 11



## Magufuli aahidi kutoa milioni 100/- kusaidia wafanyabiashara wadogo

UKURASA 3

# Panga kali waliotoa rushwa ubunge CCM

**POLEPOLE** asema watawashangaza wengi, wana orodha kamili ya wahusika ...*Endelea ukurasa wa 2*



Mgombea urais wa Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe (wa pili kushoto), akisalimiana na mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu, wakati wa Mkutano Mkuu wa ACT, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ANTHOMY SIAME**

# Membe, Maalim Seif wapitishwa kugombea urais ACT-Wazalendo

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**

**WAFUNGUA PAZIA FOMU ZA URAIS**

PAZIA la uchukuaji fomu kuwania urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilifunguliwa jana...

**UKURASA WA 5**

**MPINA AKUNWA WAVUVI, WAFUGAJI KUWEZESHWA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameisifu Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kuchochea ongezeko...

**UKURASA WA 8**

**PSSSF SASA YAANZA KUTOA FAO LA UZAZI**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umeanza rasmi kulipa fao la uzazi kwa wanachama wake...


## NDEGE KLM YAANZA TENA SAFARI TANZANIA, WATALII 117 WATUA KIA

UKURASA 3


**MICHEZO** SVEN AONDOKA, SIMBA WAGAWANYIKA MARA 2 UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiweka udongo kwenye kaburi la aliyekuwa Mtumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, marehemu Joseph Ndonjekwa katika mazishi yaliyofanyika nyumbani kwake Bunju Mabwepande jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

# Panga kali watoa rushwa ubunge CCM

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema wanachama wake wote waliojihusisha na rushwa wakati wa mchakato wa kuwania kuteuliwa ubunge na udiwani, watakatwa wakati wa kuteua watakaogombea nafasi hizo.

Vikao vya CCM vinatarajiwa kufanyika wakati wowote kuanzia sasa kuteua wanachama watakaopeperusha bendera ya chama hicho kwenye nafasi za ubunge, uwakilishi kwa upande wa Zanzibar na udiwani katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu. Katika kura za maoni zilizofanyika hivi karibuni katika maeneo mbalimbali nchini, kuliibuka madai ya baadhi ya wanachama kujihusisha na vitendo vya rushwa. Kutokana na hali hiyo, CCM imesema walioingia katika mkumbo huo watachukuliwa hatua ikiwamo kutopewa nafasi ya kugombea.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi ya CCM, Humphrey Polepole, alisema jana kuwa wanazo taarifa za watu wanachama waliotumia rushwa katika mchakato huo na kwamba watawaadabisha na kuwashangaza.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Polepole alisema katika mchakato wa awali, chama hicho kimeonyesha demokrasia ya hali ya juu hususani kwa kuendesha kwa uwazi mchakato huo japokuwa wapo wachache waliowajaribu.

"Nafahamu kwenye uchaguzi huwa kuna mambo mengi, lakini jambo moja nalijua, kwamba uchaguzi wa CCM unaongozwa na Katiba na Kanuni. Yale ambayo tumekatazwa, yasifanywe.

"Unyenyekevu wa viongozi wakati wote wa uchaguzi si jambo la mjadala. Ningependa ifahamike na napenda kuwahakikishia wana- CCM wote tuko vizuri sana na wale wachache ambao wamejaribu...jaribu.. kutujaribu, tutawashangaza. Nasema tutawashangaza," alisema.

"Chama hiki mwaka 2016 katika Mkutano wake Mkuu Maalum uliofanyika Agosti, halafu Halmashauri Kuu iliyofanyika Desemba 12 na 13, kilifanya uamuzi wa kihistoria kwa kufanya mageuzi makubwa ya kiuongozi, kioganizesheni na kiutendaji. Kazi kubwa ambayo imefanyika imekirejesha chama kwenye ramani ya siasa na uongozi wa Tanzania," aliongeza Polepole. Alisema chama hicho kitaendelea kusisitiza na kusimamia msimamo wake huo kwa kuhakikisha Katiba, Kanuni na taratibu za chama zinafuatwa na kuzingatiwa na kwamba viongozi wanaowataka ni wale tu ambao ni waadilifu.

"Ndiyo maana kwa kazi hii ya mageuzi makubwa katika maeneo hayo matatu, tunataka viongozi waaminifu, waadilifu, wachapakazi, wanaochukizwa na rushwa, na kwetu sisi rushwa ni jambo linalokataliwa kimsingi. Sasa ni vizuri wakati mwingine viongozi pia wakafundishwa adabu. Tutafundisha watu adabu kipindi hiki," alisisitiza.

Alisema katika kupata wagombea, wataweka rekodi kwamba walipata kuwapo viongozi kwenye chama ambao waliwakumbusha vikali watu ambao wanashindwa kuelewa utaratibu na waliokiuka walichukuliwa hatua.

Polepole alisema watu ambao walidhani kwamba chama hicho kutangaza kupiga vita rushwa katika mchakato wa uchaguzi ilikuwa si halisi, basi katika kipindi hiki watashangazwa.

"Katika kituo chetu kile cha taarifa za uchaguzi, tunapokea taarifa nyingi. Nasema kipindi hiki tutawashangaza watu waliodhani kwamba ni 'business as usual' (mambo ya yanakwenda kwa mazoea) inaendelea kwenye chama hiki. Wana-CCM wawe na amani, ushindi mkubwa unakuja.

"Wanachama walioomba dhamana ya uongozi ambao wamefuata na kuzingatia Katiba na Kanuni na hawakujihusisha katika makatazo na miiko, wawe na amani na watulivu. Mwenyekiti na safu yote ya uongozi, wanatambua unyenyekevu wao na sisi hatutawaangusha watu waaminifu na wenye nidhamu," alisema Polepole.

Aliongeza kuwa: "Ila wale mliopiga mazonge tutafundisha watu adabu kipindi hiki. Sipendi kusema maneno mengi kwa sababu pia unapofundishwa adabu ni vizuri ukaipata 'by surprise' (kwa kushtukiza). Unasema ee imekuwa hivyo, ndiyo imekuwa hivyo mjomba, imeisha hiyo, utafute kazi nyingine. Uongozi unaotweza misingi ya Katiba ya chama chetu hauna nafasi. Kwa hiyo wana-CCM, tulieni."

**JPM KUCHUKUA FOMU LEO**

Kwa mujibu wa taarifa ya Polepole aliyoitoa baadae jana jioni, Mwenyekiti wa Chama hicho, Rais John Magufuli anatarajia kuchukua fomu ya kugombea urais leo asubuhi.

Pia alisema wameridhika na maandalizi ya uchaguzi kwa upande wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

# Membe, Maalim Seif wapita kuwania urais

**Na Waandishi Wetu**

MKUTANO Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, umewapitisha Bernard Membe na Maalim Seif kuwa wagombea wa urais wa Tanzania na Zanzibar, mtawalia, katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu.

Wagombea hao walipitishwa jana katika mkutano huo uliofanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo mgombea urais wa Tanzania kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu.

Katika hotuba yake, Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alisema endapo watapewa fursa ya kushika dola, serikali watakayoiunda itahakikisha kila Mtanzania ana kuwa na haki ya kufurahia utanzania wake kulingana na kaulimbiu yao ya 'Kazi Na Bata'.

Alisema wanataka Watanzania wafanye kazi kwa bidii na pia wafaidi matunda ya jasho lao na wawe na raha na furaha. "Tunataka serikali zitakazoongozwa na ACT-Wazalendo, zikatae kuona vijana wa Tanzania Bara na visiwani Zanzibar wananyang'anywa fursa, wanakatishwa ndoto zao, wanakandamizwa na kufanywa watwana ndani ya taifa lao," alisema.

Zitto alisema wataandaa maisha stahiki ya uzeeni kwa kuwa na mfumo madhubuti wa hifadhi ya jamii kwa wote na kila mtu kuwa na uhakika wa bima ya afya na pensheni.

"Tuwe na elimu bora yenye kukidhi vigezo vya soko la ajira na kuwaandaa wahitimu kuvumbua na kujiajiri. Vijana wote watakaojiunga na elimu ya ufundi, watasoma bila malipo ili kuondoa kikwazo cha vijana kupata stadi na ujuzi kuendesha maisha yao," alisema.

Zitto aliongeza kuwa watahakikisha uchumi wa taifa litakaloongozwa na chama hicho utakuwa jumuishi na endelevu. "Tunataka serikali ambayo itaboresha na kuwezesha ustawi wa sekta isiyo rasmi hasa ya biashara ndogo ambazo nyingi zinafanywa na wanawake na vijana," alisema. Zitto aliendelea kusema kuwa uchaguzi wa mwaka huu ni wa kuchagua uhuru wa kweli kwa kila mtu na kuwa na maendeleo jumuishi ya watu dhidi ya maendeleo ya vitu.

Kabla ya kupitishwa, Maalim Seif aliwataka wanachama wafanye uamuzi wa hekima na busara kwa kuwachagua wagombea wazuri ambao watakwenda kuleta ushindani kwa vyama vingine.

Alisema Watanzania wanataka mabadiliko, hivyo ni lazima wapate wagombea wazuri watakaounda serikali itakayotekeleza yaliyoahidiwa na vyama.

Alisema mgombea yeyote atakayeshinda kwa uhalali Zanzibar, atampa mkono na kumpongeza na kutoa angalizo kuwa ACT-Wazalendo wakishinda, kusifanyike mbinu ya kuwanyang'anya ushindi.

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, akizungumza kwa niaba ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, alisema msisitizo wao kwa vyama ni kuheshimu sheria za nchi za vyama kuelekea uchaguzi huo.

"Uchaguzi ni ushindani, tunaelewa siasa za ushindani kuna mbwembwe nyingi. Mwenyekiti wa chama (Maalim Seif) amesema mtalinda ushindi, sisi tunasema mlinde kwa mujibu wa sheria, fanyeni mbwembwe zote za kisiasa, ila kwa mujibu wa sheria," aliagiza.

Mgombea urais kupitia CHADEMA, Lissu alisema mwaliko alioupata aliutegemea kwa sababu ACT-Wazalendo ni marafiki wa kweli na kwamba hata wasingemwalika angekwenda mwenyewe.

"Akufaaye wakati wa dhiki ndiye rafiki, kwa sababu kuna kipindi binafsi nilikuwa kwenye dhiki na nililala siku kadhaa, nilipoamka nikakuta nipo kwenye nchi nyingine, mazingira tofauti.

"Katika watu waliokuja kuniangalia miongoni ni Maalim Seif na wengine walinifuata Brussels Ubelgiji, Zitto alikuja zaidi ya mara moja na familia yake, Fatma Karume alikuja, alikuwa ananililia, nipo kitandani nikamwambia yatakwisha," Lissu alisema.

Alikiahidi chama hicho kuwa ushirikiano unaozungumzwa wataufanya ila kwa kuangalia kama maeneo watakayoshirikiana ni ndoano au salama.

■**Imeandaliwa na Romana Mallya, Mary Mshami, Fatma Mtutuma na Magdalena Haule.**

## HABARI KITAIFA

# JPM aahidi mamilioni kwa wafanyabiashara



Rais John Magufuli akila mhindi wa kuchoma aliounuua katika eneo la Dumila Darajani, alipo-simama kuzungumza na wafanyabiashara wadogo akiwa njiani kuelekea Dodoma, jana. **PICHA: IKULU**

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli amewasili Dodoma akitokea Dar es Salaam, akikubali ombi la wafanyabiashara ndogo wa Dumila mkoani Morogoro, kupanua barabara na kujenga vibanda vya kisasa vya biashara kwenye eneo hilo.

Akiwa Dumila jana wakati wa safari yake hiyo, Rais Magufuli alizungumza na wakazi wa eneo hilo ambao wanajishughulisha na biashara ndogo za kuuza mahindi ya kuchoma, mahindi mabichi, nyanya, vitunguu, mboga na bidhaa nyingine zinazozalishwa katika eneo hilo.

Rais Magufuli aliahidi kuwa serikali itatoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vibanda hivyo na pia akamwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Morogoro kufanya upanuzi wa barabara katika eneo hilo ili kupunguza msongamano wa magari.

"Nawaahidi nitawapa Sh. milioni 100 kwa ajili ya kujenga mabanda mazuri na kupanua eneo lenu la kufanyia biashara," alisema Rais Magufuli.

Awali, wafanyabiashara hao walimwomba Rais Magufuli awaongezee eneo lililoko kando ya barabara ya kwenda mkoani Dodoma, ili walitumie kufanya biashara zao.

Mmoja wa wafanyabiashara hao alisema wanaomba eneo la shamba liliko karibu na barabara ya kwenda Dodoma wapewe ili kuongeza eneo la kufanyia biashara.

Akiwa kwenye eneo hilo, Rais Magufuli alionekana kufurahia huduma ya chakula alichopewa na wenyeji wake hao, akiyasifu mahindi yao kuwa ni matamu.

Rais Magufuli ambaye ameteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwania tena urais katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, wiki hii anatarajia kuchukua fomu ya kuwania nafasi hiyo kwenye Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) jijini Dodoma.

# KLM yarejesha safari, ndege yake yatua na watalii 117 KIA

**Na Allan Isack, HAI**

SHIRIKA la Ndege la Kimataifa la Uholanzi (Royal Dutch Airlines - KLM), limerejesha tena huduma zake nchini, baada ya juzi ndege yake kutua na watalii 117 ikiwa miezi minne tangu lilipositisha huduma kutokana na baa la corona.

Juzi, shirika hilo lilizindua kurejea kwa huduma zake nchini baada ya kushuka kwa ndege yake ya abiria yenye namba za usajili Boeing 777 PH-BQB katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Jana, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, akizungumza na waandishi wa habari baada ya mapokezi ya ndege hiyo, alisema kuingia kwa watalii hao nchini kunaidhihirishia dunia kuhusu ushindi dhidi ya virusi vya corona.

"Kuja kwa watalii hawa ni ishara ya ushindi mkubwa, ni ishara njema ya amani na upendo, hivyo ninawaomba wananchi popote walipo watambue kuwa Tanzania ni sehemu salama ya utalii," alisema Mghwira.

Watalii hao waliotokea mataifa mbalimbali ya Bara la Ulaya na Asia, wako nchini kwa ajili ya kutembelea vivutio vya utalii, hasa hifadhi za taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), vilivyoko Kaskazini mwa Tanzania.

Awali, mashirika ya ndege ya kimataifa yalisitisha safari zake kwenye nchi mbalimbali duniani kutokana na tishio la maambukizi ya virusi vya corona.

Mashirika ya ndege ambayo hadi sasa yamesharudisha safari zake nchini, ni pamoja na RwandAir, Ethiopia, Qatar, Emirates na KLM.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa, kurejea kwa safari za ndege hizo, kumeithibitishia dunia kwamba wananchi wa Tanzania wameishinda hofu ya ugonjwa huo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Usimamizi na Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO), Christine Mwakatobe, ndege hiyo ya KLM iliwasili saa 2:15 usiku wa Agosti 4 mwaka huu ikiwa na watalii kutoka Ujerumani, Uingereza, Ufaransa na wengine wa Bara la Asia.

Alisema kurejea kwa safari za ndege kumetokana na serikali ya Uholanzi kuridhika na jitihada za Serikali ya Tanzania katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona.

Agosti 2 mwaka huu, Mkoa wa Kilimanjaro uliipokea ndege nyingine ya Shirika la Ndege la Rwanda (RwandAir) yenye usajili wa namba 9XR- WL.

Juni Mosi mwaka huu, walipokea ndege ya Shirika la Ethiopia na Julai 30 walipokea ndege ya Shirika la Qatar, na Agosti Mosi mwaka huu, walipokea ndege ya Crystal P4_XTL.

Akizungumza kwa niaba ya watalii wenzake waliokuja kutembelea hifadhi za taifa nchini, Getrude Boldemann, raia wa Ujerumani, alisema wamefurahishwa sana na kauli ya Rais John Magufuli kwamba Tanzani hakuna ugonjwa wa corona, ndiyo sababu wamekuja kutalii kwenye mbuga za wanyama.


**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**TENDER CANCELLATION NOTICE**

**Invitation to Bid: No. ITB/2020/SUP/018 ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENT(S) FOR THE SUPPLY OF MULTIPURPOSE SOAP**

Reference is made to the above subject Invitation to bid. Please note that the Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Tanzania, has decided to cancel and withdraw the tender ITB/2020/SUP/018 for Establishment of Frame Agreement(s) for the Supply of Multipurpose soap until further notice.

We appreciate your interest in the tender and your decision to work with us.

However, we remain interested in doing business together in future ventures should the occasion arise.

***Thank you for your cooperation.***

215844302

# DP, NRA, AAFP vyafungua pazia uchukuaji fomu urais

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

PAZIA la uchukuaji fomu kuwania urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilifunguliwa jana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), huku wagombea watatu kutoka vyama mbalimbali vya siasa wakichukua fomu na kutamba kuingia Ikulu.

Kwa mujibu wa tume hiyo uchukuaji fomu ulianza jana hadi 25, mwaka huu katika Ofisi za NEC zilizopo jijini hapa.

Wagombea hao walianza kuwasili katika Ofisi za NEC kuanzia saa 4:30 asubuhi, ambapo mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia AAFP, Seif Maalim Seif alikuwa wa kwanza kufika akiwa ameambatana na Mgombea Mwenza wake, Rashid Ligania Rai na wanachama.

Mgombea wa pili wa DP, Philipo Fumbo aliwasili saa 5:30 asubuhi bila mgombea mwenza, Zainab Juma Hamisi na wapambe wake wanne.

Mgombea wa tatu wa NRA, Leopord Mahona aliwasili saa 6:30 mchana akiwa na wapambe wawili bila mgombea mwenza, Hamis Ali Hassan.

Wagombea hao walikabidhiwa fomu hizo na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage.

**KAULI YA MGOMBEA AAFP**

Akizungumza nje baada ya kukabidhiwa fomu, mgombea huyo aliwaahidi Watanzania kuwa ataleta mabadiliko ya kweli.

"Nakwenda kutafuta wadhamini na kurejesha fomu, hatua itakayofuata ni kuingia Ikulu, tuna imani na Tume katika kusimamia suala zima la uchaguzi, tunahitaji mabadiliko ya kweli yanayoathiri mwananchi mmoja mmoja kwa kila siku, AAFP tunaamini tuna uwezo, sababu na utayari wa kuleta hali bora zaidi kuliko ilivyosasa iwe kiuchumi, kijamii na muktadha mzima wa kimaendeleo," alisema.



Mgombea Urais wa AAFP, Seif Maalimu Seif




Mgombea Urais wa DP, Philipo John Fumbo



Mgombea Urais wa NRA, Leopold Lucas Mahona

**MGOMBEA DP ANENA**

Mgombea Fumbo, alisema chama hicho ndio kinachosikilizwa kwa kuwa ni cha walala hoi, hivyo watafanya maajabu ya 'Njiti ya kiberiti kuwasha msitu'.

"Tunatakiwa tukatafute wadhamini, na kwenda mikoani sina shaka kwa kuwa nina wadhamini wa kutosha nitamaliza zoezi hili haraka maana chama hichi kina mila tofauti na vyama vingine vya siasa, hivyo baada ya kupata wadhamini na kurudisha fomu, DP itawasha moto maana baada ya kuteuliwa ni saa ya ukombozi," alisema.

**MGOMBEA NRA AFUNGUKA**

Mgombea NRA, Mahona alisema huo ni mwanzo wa utumishi wake kwa nchi na ni safari nzuri na ya matumaini kwa Watanzania ambayo itawahakikishia kuwa yaliyopita sasa yamepita.

Alitoa wito kuwe na uchaguzi huru ili Watanzania wapate kiongozi wanayemtaka.

**UFAFANUZI WA NEC**

Akitoa maelezo ya awali kabla ya kukabidhiwa fomu hizo, Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Charles Mahera, alisema watatakiwa kudhaminiwa na wapigakura wasiopungua 200 ambao wamejiandikisha kupiga kura katika kila mkoa kwenye mikoa 10 na kati ya hiyo angalau miwili kutoka Zanzibar.

**RATIBA UCHUKUAJI FOMU**

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Tume hiyo, leo wagombea wa UPDP na Demokrasia Makini watachukua fomu.

Pia, Agosti 7, mgombea wa Chama cha ADC atachukua fomu huku wa CHADEMA atachukua Agosti 8, mwaka huu.

Agosti 11, wagombea wa UMD na CUF na Agosti 12 ni zamu ya CCK.

# Meya ampongeza JPM kuondoa hofu corona

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Abdalah Mtinika, amempongeza Rais John Magufuli kwa mikakati imara ya kukabiliana na tishio la corona na kuwapa ujasiri wananchi kutokuwa na hofu ya virusi hivyo.

Mtinika alitoa pongezi hizo jana jijini Dar es Salaam wakati alipozungumza katika hafla ya uzinduzi wa kampeni iliyoandaliwa na WaterAid inayolenga kupambana na magonjwa ambukizi ambayo chanzo chake ni uchafu unaotokana na kutokunawa kwa majisafi na sabuni.

Meya huyo alisema kunawa mikono kutaepusha siyo tu kupata virusi vya corona, bali pia magonjwa zaidi ya saba ambayo silaha ya kuyaangamiza ni usafi wa mwili hasa kunawa mikono mara kwa mara kwa maji yanayotiririka.

"Unaponawa mikono mara kwa mara kwa maji yanayotiririka, unaepukana na magonjwa mengi yanayoambukizwa kama vile corona, kipindupindu, kichocho na magonjwa mengine ambayo chanzo chake ni kutokunawa mikono na sabuni," alisema.

Meya huyo pia aliishauri taasisi hiyo kufika mbali zaidi kuifikisha elimu hiyo kwa jamii hususani mitaani na kwa wanafunzi wa shule mbalimbali nchini ili elimu ienee zaidi nchini.

"Ninawashauri WaterAid kwamba uzinduzi wa kampeni hii ya 'Usichukulie Poa Unategemewa', ihusishe na utoaji wa elimu kuanzia mitaani pamoja na shuleni ambako ndiko kuna kizazi cha baadae na hilo litasaidia sana katika kuhakikisha tunafika mbali na kampeni hiyo.

"Hatuwezi kuifikisha elimu kote kwa kutumia waandishi wa habari tu, ila utoaji wa elimu mtaa kwa mtaa ni muhimu zaidi," kiongozi huyo alisisitiza.

Mkurugenzi Mkazi Mradi wa WaterAid, Anna Mzinga, alisema wataendelea kuiunga mkono serikali katika kukabiliana na magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya uchafu unaotokana na watu kutokuwa na utamaduni wa kunawa kwa maji tiririkia na sabuni.

Alisema kampeni hiyo iliyozinduliwa jana imewashirikisha wasanii mbalimbali na mchezaji wa mpira wa miguu, Juma Kaseja watakaotoa elimu kwa jamii katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Geita na Zanzibar.

"Kampeni hii itaendelea hadi Januari na itahusisha kusambaza na kueneza ujumbe wa mabadiliko ya tabia ya usafi kupitia vyombo vya habari pamoja na matukio ya ushiriki wa jamii," alisema Mzinga.

"Magonjwa haya ni mengi sana na serikali inajitahidi kupambana na magonjwa ambukizi kwa lengo la kufanya kila mtu awe na afya imara, aweze kuendelea na shughuli za kulijenga taifa letu, hivyo tupo nao bega kwa bega kwa kuwa sisi ni wadau wa maji," aliongeza.

Balozi katika kampeni hiyo, Mrisho Mpoto, alisema ni aibu kubwa kuona mtu anapata maradhi kutokana na uchafu na kutokunawa mikono kwa majisafi na sabuni.

# Mwakyembe aiagiza BAKITA kudhibiti opotoshaji Kiswahili

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amelitaka Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), kuwasajili wafasiri, wakalimani na wataalamu wa lugha ya alama, ili kuboresha matumizi fasaha ya Kiswahili na kuzuia upotoshaji.

Pia, amewataka BAKITA kuwabana wachapishaji wa vitabu kabla ya kuingia sokoni mpaka vipate ithibati, wamiliki na walimu wa vituo vya kufundishia Kiswahili kwa wageni kupewa vyeti vya utambuzi.

Alitoa maagizo hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kanuni za sheria mpya za BAKITA. "Vitabu vyote vipate ithibati, vitakavyobainika havina ithibati viondolewe na muhusika achukuliwe hatua," alisema Dk. Mwakyembe.

Alisema hatua ya kutoa vyeti kwa vituo vya kufundishia Kiswahili kwa wageni itasaidia kuwapo kwa vituo vyenye ubora na kuwaondoa watoa huduma wasio na uwezo.

Naye, Kaimu Mtendaji wa BAKITA, Consolata Mushi akizungumzia kuhusu kanuni hizo, alisema lengo ni kuliwezesha BAKITA kusimamia shughuli za maendeleo na matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha, kuhimiza, kuzuia upotoshaji wake.

"Licha ya kanuni hizi kuwalenga watumiaji wote wa lugha ya Kiswahili, hata hivyo kuna makundi na wadau mbalimbali ambao wataguswa moja kwa moja na masharti ya kanuni hizi," alisema Mushi. Mushi alisema wamiliki na walimu wa kufundisha Kiswahili kwa wageni watapaswa kupata vyeti vya utambuzi kutoka BAKITA, kupitisha mitaala na vitabu.

Alisema waandaaji wa matamasha ya Kiswahili kwa wageni watapaswa kuomba idhini ya kuandaa tamasha au shindano la Kiswahili kwa BAKITA.

Pia, vyombo vya habari vitapaswa kupata tafsiri rasmi kutoka BAKITA ya tangazo au habari iliyo katika lugha ya kigeni, kushiriki katika semina za mafunzo yanayohusiana na lugha ya Kiswahili.

Alisema kwa wafasiri, wahariri, wakalimani na wataalamu wa lugha ya alama, watapaswa kujisajili katika kanzidata ya BAKITA na kupata cheti cha utambuzi, kushiriki katika semina za mafunzo yanayohusiana na lugha ya Kiswahili yaliyoandaliwa na BAKITA.

"Waratibu na waandaaji wa mikutano watapaswa kupata wafasiri, wakalimani na wataalamu wa lugha ya alama kutoka BAKITA. Vilevile watafiti katika lugha ya Kiswahili nao watalazimika kupata kibali, wachapishaji wa vitabu kupata ithibati ya vitabu kutoka BAKITA kabla ya kuchapisha na kusambaza vitabu vyao," alisema Mushi.

Mushi alisema wazalishaji wa bidhaa viwandani watapaswa kupata tafsiri ya lugha ya Kiswahili ya maelekezo ya matumizi ya bidhaa zao, kuwasilisha maandiko ya lugha ya Kiswahili yanayohusu bidhaa au huduma kutoka BAKITA kwa ajili ya kuhaririwa.

Kwa mujibu wa Mushi, kanuni hizo zitawahusu watumiaji wa lugha ya Kiswahili pamoja na wazalishaji wa bidhaa viwandani, wachapishaji vitabu, vyombo vya habari, wasanii wakalimani na wataalamu wa lugha za alama.

Wengine ni wamiliki na walimu wa vituo vya kufundishia Kiswahili kwa wageni, waandaaji wa matamasha, mashindano ya Kiswahili, wahariri, wataalamu wa lugha ya alama, waratibu wa waandaaji wa mikutano, watafiti katika lugha ya Kiswahili pamoja na waandishi chipukizi.

# Mpina akunwa wavuvi, wafugaji kuwezeshwa

**Na Mwandishi WETU**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina ameisifu Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa jitihada za kuchochea uongezekaji wa tija katika uzalishaji na mapato ya Watanzania wanaojiajiri katika sekta ya mifugo na uvuvi.

Akizungumza katika kikao kazi kilichopitia utekelezaji wa malengo na kuzingatia mafanikio yaliyopatikana tangu kikao cha mwisho kilichofanyika Agosti 10, mwaka huu.

Waziri Mpina alisema kuwa TADB imekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na mabenki washirika kuwakopesha wadau wa sekta ya uvuvi na ufugaji na kwa hiyo kizifanya sekta hizo ziwe na maana kwa Watanzania.

"Ninachukua fursa hii kuipongeza TADB kwa jitihada zake za kuisaidia sekta hizi za mifugo na uvuvi kwa kuwa hivi sasa wadau wa sekta hii wanawezeshwa kwa kupatiwa mikopo ya kuendesha shughuli zao," alisema Mpina.

Alisema amefarijika kuona sekta kama ya uvuvi ambayo haikupewa kipaumbele siku za nyuma lakini sasa TADB imejitosa na inawakopesha wadau wa sekta hiyo na kusema hilo ni moja ya mambo ya kupongezwa na kuungwa mkono na kila mpenda maendeleo.

Aidha ameisifu benki hiyo kwa kuongeza mnyororo wa thamani kwa bidhaa zinazotokana na uvuvi na ufugaji kwa kufufua viwanda vikubwa vya maziwa, kikiwemo kiwanda cha maziwa cha ushirika mkoani Njombe.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, amekieleza kikao hicho kuwa benki hiyo imejipanga kikamilifu kuhakikisha inatoa mikopo kwa waombaji wengi zaidi ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

"Hadi hivi sasa benki yetu imepokea maombi ya zaidi ya Sh. bilioni 85.5. Kati ya hizo, zaidi ya bilioni 27 ndio zimeidhiniswa na benki huku zingine zikiendelea kushughulikiwa alisema.

Aliongeza kuwa Sh. bilioni 27 zilizotolewa kama mikopo, Sh. bilioni 3.425 zimepitia Mfuko wa Dhamana kwa Wavuvi na Wafugaji Wadogo, ambao unawawezesha wafugaji na wavuvi kukopa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zao.

"Fedha hizi tunazowakopesha zinawasaidia sana wavuvi na wafugaji kuendesha shughuli zao. Natoa rai wananchi wajitokeze kwa wingi kwani serikali imedhamiria kuwainua na sisi tupo na tutashirikiana nao kuhakikisha wanahudumiwa ipasavyo na kwa wakati," aliahidi Justine.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge (kushoto), akionyeshwa michoro ya ujenzi ya machinjio ya Vingunguti, kutoka kwa msimamizi wa mradi wa ujenzi huo, Mhandisi Mbuvuga Matamwe, alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo mkoani humo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BRELA, watafiti mbegu atamba Nanenane

**Na Renatha Msungu,** SIMIYU

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), unayatumia maonyesho ya wakulima, maarufu Nanenane, kutoa huduma ya kusajili leseni ya mifugo na wakulima katika Viwanja vya Nyakabindi wilayani Bariadi mkoani Simiyu.

Akizungumza katika maonyesho hayo jana, Ofisa Biashara wa wakala huo, Paul Peter, aliwataka wakulima na wafugaji wa mkoa huu kutumia fursa za maonyesho hayo kupata huduma hiyo.

"Niwatake wakulima na wafugaji wa mkoa huu, watumie fursa ya maonyesho haya kupata leseni ya biashara ya kusafirisha mifugo na mazao kwa wakulima, ili wafanye biashara zao kwa uhuru," alisema.

Alibainisha kuwa kwa wafugaji, kabla ya kwenda BRELA, wanatakiwa wawe wamejisajili katika Bodi ya Nyama ili kupatiwa vielelezo muhimu vya kukatiwa leseni.

"Tunatoa leseni kwa wafanyabiashara wanaosafirisha mifugo na mazao yao ndani na nje ya nchi, BRELA tupo hapa kutoa huduma hiyo bure kabisa," alisema.

Wakati BRELA wakitoa huduma hiyo, Kituo cha Utafiti wa Mbegu za Mboga nacho kinayatumia maonyesho hayo kutoa elimu kuhusu kilimo cha mboga na viungo ambacho kwa sasa kina soko kubwa duniani.

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika wa kituo hicho, Dk. Gabriel Rugalema, alisema kuwa kilimo cha viungo kina faida kubwa kwa kuwa mahitaji yake ni makubwa kwa sasa duniani kote.

Alisema kuwa kwa kutambua hilo, kituo chao kimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha wakulima wanaendesha kilimo hicho kwa utaalamu mkubwa akifafanua: "Tunajitahidi kuhakikisha wakulima wanaelewa kilimo hicho."

Wakulima waliohudhuria maonyesho hayo walisema wameona umuhimu wa kilimo cha mboga, akiwamo Husna Mohamed, aliyeweka wazi kuwa anaendesha maisha kupitia kilimo hicho..

# Bashungwa ashauri wajasiriamali kukopa fedha kwenye taasisi rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ametoa wito kwa wajasiriamali wanawake na vijana kutohofia kuomba mikopo kwenye taasisi kubwa za fedha zikiwamo benki ili kujiepusha na mikopo isiyo rasmi ambayo imekuwa ikiwagharamu kwa kuwatoza riba kubwa na hivyo kuwarudisha nyuma kiuchumi.

Waziri Bashungwa alitoa wito huo jana wakati akifungua Kongamano la Biashara na Kilimo lililoandaliwa na Jumuiya ya Wafanyabiashara Wanawake na Vijana (TABWA) kwa kushirikiana na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) linalofanyika kwenye Viwanja vya Maonyesho ya Kilimo ya Nanenane yanayofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu.

Pamoja na kuipongeza Benki ya NBC kwa mchango wao katika kutoa mikopo ya biashara kwa wanawake na vijana nchini, Waziri Bashungwa aliziomba pia taasisi za fedha nchini kusikiliza vilio vya wanawake na vijana ambao wamekuwa wakilalamikia ugumu wa masharti yanayoambatana na mikopo hiyo ambayo yanakuwa kikwazo kwao.

"Licha ya taifa kuwa na idadi kubwa ya wanawake wenye ujasiri wa kubuni na kuendesha biashara, kasi ya ukuaji wa mitaji yao bado ni finyu.

Inafahamika chanzo kikuu cha mitaji yao ni mikopo ya kibiashara ila changamoto inabaki kuwa wengi wao hawana mikopo kutoka kwenye taasisi rasmi za kifedha na matokeo yake wanaangukia kwenye mikopo isiyo rasmi inayowanyonya sana kwa riba kubwa ndio maana nimeomba benki kubwa ziwasaidie pamoja na kuwaelimisha kama ambavyo Benki ya NBC wanavyofanya...nawapongeza sana," alisema.

Kwa upande wake Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki kutoka Benki ya NBC, Jonathan Bitababaje, alisema pamoja na kuwajengea uwezo wa kifedha na kiufanisi kwenye biashara benki hiyo imejipambanua kama kituo kimoja chenye mahitaji yote ya wajasiriamali kwa kutoa huduma mahususi na maalum zinazoakisi mazingira ya biashara ya ndani kwa lengo la kukuza na kuendeleza sekta ya wajasiriamali wakiwapo wanawake nchini.

"Katika kuhakikisha hilo, benki kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo TABWA na TANTRADE tumeendeleza kliniki kama hizi za biashara pamoja na vilabu vinavyofahamika kama 'NBC-Club' ambavyo vinawaunganisha wajasiriamali na kuwawezesha kufanya safari za kibiashara, huduma za bure za ushauri wa kibiashara na upendeleo maalum katika baadhi ya huduma, hatua ambayo inalenga kuwajenga zaidi kibiashara na kiuchumi kwa jumla," lisema.

Mkurugenzi wa TABWA, Doreen Mawala, alisema utayari wa wanawake kuomba mikopo unaathiriwa na sababu kadhaa ikiwamo viwango vikubwa vya riba vinavyotozwa na benki kwa mwaka, huku pia akitaja suala la dhamana ya mali kuwa ni kikwazo, kwa kuwa wengi wao hawana mali kama nyumba au ardhi za kuweka rehani ili wapate mikopo.

"Kwenye hili tunawashukuru sana Benki ya NBC, TANTRADE, BRELA, TRA, TBS, TMDA, SIDO,GS 1, UDSM na wengine wengi.


## KUMBUKUMBU



*Magdalena E. Mwakasege*

Ilikuwa huzuni kubwa sana
pale ulipotutoka Agosti 6/2019
lakini sasa tunajua wewe ni malaika mlinzi kwetu.
Unakumbukwa Sana na mama yako Elesia
Mulenga, watoto wako Steward Davidson,
Happy, Vitus, Vanessa, Vernon, Godfrey, Glory,
Daines na Destiny pamoja na Kaka na dada
zako ambao wanakukumbuka sana.

***Ayub 1:21 Ameen***

115846302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Ushauri wa Bashungwa wanawake, vijana kukopa taasisi rasmi ufanyiwe kazi*

MAKUNDI maalum ya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yamekuwa yakikumbana na vikwazo vingi katika kufanya shughuli zao za kujitafutia riziki.

Makundi haya yamekuwa yakiitwa ya watu waliosahaulika, kutokana na mazingira na changamoto yanazokumbana nazo, ikiwamo kupata mikopo. Pamoja na vikwazo vingine vinavyowakwamisha kupata mikopo hiyo, lakini kubwa ni kutokuwa na dhamana kwa ajili ya kukopeshwa na benki pamoja na taasisi rasmi za kifedha.

Utaratibu uko wazi kuwa anayetaka kukopa benki au taasisi zingine rasmi za kifedha, ni lazima aweke dhamana hususan mali zisizohamishika kama nyumba, kiwanja, shamba nakadhalika, masharti ambayo ni magumu kwa wananchi wanyonge, yakiwamo makundi hayo. Kwa kulitambua tatizo hilo, serikali ilijaribu kupunguza ukubwa wa tatizo hilo kwa kuziagiza halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya kuyakopesha makundi hayo kwa lengo la kuyawezesha kujikimu kimaisha kupitia shughuli za ujasiriamali.

Kwa mujibu wa maelekezo ya serikali, kila halmashauri inatakiwa kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuyakopesha makundi hayo, ingawa uzoefu umeonyesha kuwa upatikanaji wa fedha kwenye halmashauri nyingi ni changamoto.

Halmashauri nyingi zimekuwa zikilalamika kushindwa kutenga fedha za mfuko huo, ambapo sababu kubwa ni kuwa na vyanzo vichache vya mapato ya ndani pamoja na baadhi ya vyanzo vingine kuchukuliwa na Serikali Kuu.


Kutokana na hali hiyo makundi haya yanakwama kupata mikopo inayostahili, hivyo kupata kidogo, wakati mwingine hata hicho kidogo kuchelewa kukipata na wakati mwingine kukosa kabisa. Njia iliyochukuliwa na wajasiriamali hao ni kujaribu kutafuta mikopo kwa njia zingine, ikiwamo kwa wakopeshaji binafsi ambao wametapakaa mitaani, huku wakiwakopesha wahitaji wa riba kubwa kupitiliza, ambazo mwishowe ni kuwafilisi wakopaji.

Serikali imeshaliona tatizo hilo ambalo limesababisha makundi ya wajasiriamali kukwama baada ya mali zao kufilisiwa na wakopeshaji kutokana na riba kubwa za marejesho ya mikopo. Jana Waziri Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, aliwataka wajasiriamali wanawake na vijana kutohofia kuomba mikopo kwenye taasisi kubwa za fedha zikiwamo benki ili kujiepusha na mikopo isiyo rasmi ambayo imekuwa ikiwagharamu kwa kuwatoza riba kubwa, hivyo kuwarudisha nyuma kiuchumi.

Waziri Bashungwa alitoa wito huo wakati akifungua Kongamano la Biashara na Kilimo lililoandaliwa na Jumuiya ya Wafanyabiashara Wanawake na Vijana (TABWA) kwa kushirikiana na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kwenye Viwanja vya Maonyesho ya Kilimo ya Nanenane yanayofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu . Waziri Bashungwa aliziomba pia taasisi za fedha nchini kusikiliza vilio vya wanawake na vijana, ambao wamekuwa wakilalamikia ugumu wa masharti yanayoambatana na mikopo hiyo, ambayo yanakuwa kikwazo kwao.

Kwa mujibu wa Bashungwa, licha ya Tanzania kuwa na idadi kubwa ya wanawake wenye ujasiri wa kubuni na kuendesha biashara, kasi ya ukuaji wa mitaji yao bado ni finyu, na kwamba inafahamisha dhahiri kuwa chanzo kikuu cha mitaji yao ni mikopo ya kibiashara, ila changamoto inabaki kuwa wengi wao hawana mikopo kutoka kwenye taasisi rasmi za kifedha na matokeo yake wanaangukia kwenye mikopo isiyo rasmi inayowanyonya sana kwa riba kubwa. Alisema ndiyo maana ameziomba benki kubwa ziwasaidie pamoja na kuwaelimisha. Sisi tunaiona changamoto hii kuwa inahitaji mipango, mikakati na nguvu ya pamoja kwa ajili ya kukabiliana nayo. Jambo la msingi na la kupongeza ni wazo aliloliibua Waziri Bashungwa, hivyo kilichobaki ni wizara na taasisi za serikali kuketi pamoja kuangalia utekelezaji wake ili kuwakwamua wajasiriamali wetu wanawake na vijana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Maji umbali usiozidi mita 400, unapunguza ukatili kijinsia*

SERA ya Maji ya Mwaka 1991, ililenga kuhakikisha ifikapo mwaka 2000, wananchi wote wawe wamekwishapata majisafi na salama, kwa kiwango cha kikidhi mahitaji yao.

Maji yalitakiwa yapatikane umbali usiozidi mita 400 ifikapo mwaka 2002, ili kuwaondolea usumbufu wa kupata huduma hiyo, kwa kutembea umbali mrefu ambao wakati mwingine si salama kwao.

Hata hivyo, lengo la sera hiyo bado halijatimia hasa kwenye baadhi ya vijiji, hali inayosababisha wanawake na wasichana kutembea umbali mrefu, kufuata huduma hiyo muhimu.

Pamoja na juhudi za serikali kuwapatia wananchi maji, kuna dokezo la kiuchambuzi kwamba, sera ilitajwa kuwa na upungufu wake, ikiwamo kutokushirikisha sekta binafsi na wananchi wakati wa kuipanga, kutekeleza na usimamizi wake vijijini.

Mengine yanahusu uwekaji msisitizo katika usambazaji, kuliko utunzaji, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali maji katika maisha ya binadamu, hali kadhalika kukosekana mikakati mahsusi ya kuitekeleza.

Kutokana na hali hiyo, serikali iliandaa sera nyingine mwaka 2002 iliyozingatia kuziba mianya ya upungufu uliojitokeza katika sera ya awali, lengo ni kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwa wingi.

Taarifa za Wizara ya Maji inaeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kumaliza kero zinazojitokeza, ikiwamo watumiaji kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Mtazamo uliomo katika mkakati huo, unaelezwa kuwa muhimu zaidi katika upatikanaji maji kwa wingi, jambo linaloelezwa litasaidia kuwanusuru kinamama na mabinti ambao ndio waathirika wa kwanza. Inapotokea maboresho katika eneo hilo, ina maana ya faraja kubwa, kundi hilo kuwa mbali na hatari ya kukumbwa na ukatili wa kijinsia, pindi wanapotembea umbali mrefu kufuata maji.

Uzoefu unaonyesha kwamba kundi hilo la wanajamiii pindi wanapotembea umbali mrefu kufuata maji, kuna wakati wanapita katika mazingira hatari rahisi kukumbana na ukatili kama ubakaji na kuhatarisha maisha yao.

Hivyo, juhudi zinahitajika kuhakikisha maji yanapatikana nchi nzima katika umbali uliopendekezwa na sera, chini ya mita 400. Hapo inabeba maana kwamba, kinahakikishwa usalama wa afya za wanawake na wasichana kuliko walivyo sasa.

Tunafahamu kuwapo juhudi mbalimbali zinachukuliwa na serikali kuhakikisha maji yanapatikana, ikiwamo kuanzisha Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (Ruwasa), kasi ya usambazaji huo iongezwe.

Upatikanaji maji katika maeneo jirani na wananchi, utasaidia kuwaondolea hatari ya kukumbana na vitendo vya ukatili, hasa kutokana na ukweli kwamba dunia ya leo, baadhi ya binadamu hawana huruma.

Hapo RUWASA wana wajibu wa kusanifu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maji vijijini, kutafiti yanayohusu maji ardhini, kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa, kusajili na kuviwezesha vyombo vya watumiaji maji vijijini.

Vilevile, kuna jukumu la kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika maendeleo ya sekta ya maji vijijini na kumshauri Waziri wa Maji, yanayohusu uendeshaji sekta ya maji vijijini, kwamba yafanyike kwa ufanisi ili kuharakisha upatikanaji wake.

Kwa wanaoishi vijijini watakuwa wanaelewa vyema wanachokieleza, kwani upatikanaji maji kwenye maeneo yao bado ni tatizo linalohitaji kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. Kukosa maji katika baadhi ya maeneo ya vijijini na mijini unaibua wadau wa kutetea haki za wanawake na wasichana, kukihimizwa haja ya bajeti yake kuwa na mrengo wa kijinsia. Huduma ya maji inahitaji bajeti ya mrengo wa kijinsia, kwa vile wenye jukumu la kuchota maji katika familia ni wanawake, hivyo maji yanapatikana katika maeneo karibu ni nafuu kwao.

Ofisa Habari wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Monica John, anaunga mkono kwamba asasi yao inaamini kukiwapo bajeti ya aina hiyo inayowagusa wanawake, ni ishara ya ukombozi kwao.

Ukweli unaotawala ni kwamba, katika harakati yoyote ya kusaka maji ya kutumia, mzigo mkubwa unawaangukia kinamama, wanaogawanyika katika makusudi makuu mawili ya wasichana na watu wazima, wote wanatembea umbali mrefu kufuatilia na ndipo inajenga hoja ya sasa yapatikane jirani, umbali usiozidi mita 400.

# Kesi ya kina Idriss yasubiri mazungumzo kukiri kosa

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri umesema unafanya mazungumzo na washtakiwa Idriss Sultan (27) na Innocent Maiga, wanaokabiliwa na kesi ya kushindwa kusajili laini ya simu inayomilikiwa na mtu mwingine kuhusu kukiri makosa dhidi ya tuhuma hizo.

Madai hayo yametolewa na Wakili wa Serikali Kija Luzunbana kesi hiyo ilipopangwa kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Hakimu alisema mahakama yake inasubiri majibu ya mazungumzo ya pande hizo mbili na kuamuru wayawasilishe mahakamani kabla ya Agosti 27, mwaka huu.

Alisema kesi hiyo iko kwenye hatua ya kuita mashahidi kama mazungumzo yakikamilika mahakama yake ipelekewe majibu.

Mapema mahakamani hapo, ilidaiwa kuwa kati ya Desemba 1, 2019 na Mei 19, 2020 katika eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, Idriss alitenda kosa la kushindwa kufanya usajili wa laini ya simu inayotumiwa na mtu mwingine.

Ilidaiwa kuwa katika kosa hilo mshtakiwa alitumia kadi ya simu iliyomilikiwa na Maiga bila kuripoti kwa mtoa leseni.

Katika shtaka la pili mshtakiwa Maiga anadaiwa kutenda kosa la kushindwa kutoa taarifa ya mabadiliko ya kadi ya simu kutoka kwake kwenda kwa Idriss kosa analodaiwa kulitenda kati ya Desemba 1, 2019 na Mei 19, mwaka huu eneo la Mbezi Beach, Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Pia alidai Mei 5, mwaka huu, Mkuu wa Upelelezi Kinondoni alipewa taarifa kwamba Idriss anatumia kadi ya simu ya Vodacom ambayo haijasajiliwa kwa jina lake na alitakiwa kuripoti Kituo cha Polisi Oysterbay na alifanya hivyo.

Ilidaiwa polisi walienda kufanya upekuzi nyumbani kwa Idriss na kubaini uwepo wa laini hiyo ya simu na kwamba ilikuwa akiitumia kwa mawasiliano yake ya kila siku licha ya kusajiliwa kwa jina la Maiga.

Ilidaiwa Idriss alikiri kutumia kadi hiyo ya simu ambayo ilikuwa ikimilikiwa kabla na Maiga na alikiri kuitumia tangu Desemba, mwaka jana.

Mshtakiwa Maiga alidaiwa kukiri kumiliki kadi hiyo na alimpatia Idriss aweze kuitumia na alikiri kutoripoti kwenye mamlaka kuhusu mabadiliko ya kadi hiyo.

Washtakiwa hao ambao wanawakilishwa na Wakili Jebra Kambole na Maria Mushi, walikiri maelezo yao binafsi pamoja na mashtaka yanayowakabili mahakamani hapo na kukana maelezo ya mashtaka.

Upande wa mashtaka ulidai utaleta mashahidi 15 na kama watahitaji kuongeza au kupunguza wataieleza mahakama na wataeleza idadi ya vielelezo watakavyokuwa navyo kesi itakapoendelea.

# Mfanyabiashara amlilia Waziri Mkuu

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Gerald Ibrahim, maarufu kama Serikali, amemwangushia kilio Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa amsaidie kutoa maelekezo alipwe deni lake la Sh. milioni 15 kutoka kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma.

Serikali na wenzake watano, wakazi wa kijiji cha Mpeta, wilayani humo, wanaomba Waziri Mkuu awasaidie kulipwa fedha hizo baada ya kuongoza msako wa silaha mbili ikiwamo bunduki aina ya SMG na bastola pamoja na kutuliza ghasia.

"Miaka mitatu sasa tangu mwaka 2018 nilipopewa kazi na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa nilitumia fedha hizo kufanikisha upatikanaji wa silaha na zilipatikana. Namwomba Waziri Mkuu anisaidie kwani nilikopa pesa hizo kutoka kwa watu mbalimbali wananidai sasa," alisema.

Mfanyabiashara huyo alisema alisema kati ya Oktoba 16 na 17, 2018 yalitokea mapigano kati ya wananchi wa kijiji hicho na askari polisi na katika mapigano hayo, silaha mbili zilipotea hali iliyosababisha uongozi wa mkoa na wilaya kumtuma kufanya kazi hiyo kutokana na kukubalika na wananchi.

"Nilifanikiwa kutuliza ghasia, tuliitafuta silaha tukafanikiwa kuzipata na kuzikabidhi kwa uongozi wa wilaya na baada ya hapo niliandika maombi ya kulipwa fedha," alisema.

Pia alisema kati ya Septemba 13 na 14, mwaka jana, Waziri Mkuu alifanya ziara mkoani Kigoma, lakini hakufanikiwa kumwona kumweleza kilio chao.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa (kulia), akimsikiliza Verimund Kapinga (kushoto) kutoka kampuni ya ETC Agro, ambayo ni mteja wa Benki ya NBC na mdau wa kilimo wakati alipotembelea banda la benki hiyo, kwenye viwanja vya maonyesho ya kilimo ya Nanenane katika Uwanja wa Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu. Katikati ni Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TBS yatumia Nanenane kusajili majengo

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) kupitia ofisi ya Kanda ya Kaskazini imeanza kutoa huduma ya kusajili majengo wakati wa maonyesho ya Nanenane ikiwa ni kwa mara ya kwanza kufanya hivyo.

Ofisa Masoko Mwandamizi wa TBS, Gladness Kaseka, alisema hayo wakati wa maonyesho Kanda ya Kaskazini yanayofanyika katika viwanja vya Themi, jijini hapa.

Alisema TBS ni moja ya wadau wakubwa katika maonyesho hayo kwa kuwa viwango ni suala linalotakiwa kuzingatiwa na wakulima, wavuvi na wafugaji katika mnyororo wa kuongeza thamani wa bidhaa zao.

Kwa mujibu wa Kaseka, watu wakizalisha bidhaa zenye viwango itawaongezea imani wanunuzi na pia kuwawezesha kupata masoko ndani na nje ya nchi.

Naye Mkaguzi wa TBS, Anderson Msumanje, alitoa wito kwa wenye hoteli, migahawa, maghala ya chakula, maduka ya vipodozi na chakula na maduka makubwa kufika katika maonyesho hayo kwa kuwa TBS watatoa huduma ya kusajili majengo papo hapo.

"Wateja wote tunawakaribisha kupata huduma hii. Cha muhimu waje na nakala ya TIN (namba ya utambulisho wa mlipakodi) na leseni ya biashara.

Huduma hii kwa kawaida inapatikana kupitia mfumo wa kimtandao (OAS) unaopatikana kupitia tovuti ya TBS ( www.tbs.go.tz), mteja itampasa kujisajili mwenyewe kupitia mfumo," alisema.

Alisema TBS imetumia fursa hiyo ya Nanenane ili wateja ambao wanakutana na changamoto katika kujisajili ili kuhakikisha wanafanikisha usajili wao na kuepuka usumbufu wa kufanya biashara isiyo rasmi.

Kaimu Mkuu wa Kanda wa TBS, Stanford Matee, alisema mpaka sasa kwa kanda hiyo, TBS imeshatoa leseni 446 na kuna zaidi ya maombi 1,500 ambayo yako kwenye mchakato.

"Pia niwakumbushe wajasiriamali wadogo kuwa kupata leseni ya kutumia alama ya ubora ni bure kabisa, wanachohitaji ni kupata barua ya utambulisho kutoka katika ofisi ya SIDO na kutuma maombi katika ofisi yoyote ya TBS iliyopo karibu nayo," alisisitiza Matee.



Muuza bidhaa za Vodacom, Thomas Jacob (kushoto), akitoa maelezo kuhusu ubora wa simu za Smart Kitochi kwa wateja, waliotembelea banda la kampuni hiyo, katika maonyesho ya Nanenane, mkoani Simiyu jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aipongeza NMB elimu kwa wakulima

**Na Happy Severine,** BARIADI

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Inoccent Bashungwa, ameipongeza benki ya NMB kwa utoaji wa elimu ya kifedha bure kwa wajasiriamali mbalimbali wakiwamo wakulima, wavuvi na wafugaji kwenye maonyesho ya Nanenane kitaifa katika viwanja vya Nyakabindi mjini hapa.

Amesema jambo ambalo linalofanywa na benki hiyo ni muhimu sana hasa kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ambao wana uhitaji mkubwa wa elimu ya usimamizi wa fedha.

Bashungwa alisema hayo jana baada ya kutembelea banda la benki hiyo na kufurahishwa kukuta wakulima, wafugaji na wavuvi wamejitokeza kwa wingi kupata elimu hiyo.

Alisema lengo kubwa la serikali kuanzisha maonyesho hayo ni kutaka wananchi walioko kwenye sekta ya kilimo kupata teknolojia za kuwawezesha kuongeza tija kwenye uzalishaji wao na mikopo. "Wamekuwa wakipata hizi teknolojia, lakini bado tatizo lipo kwenye kujua wapi wapate mikopo, lakini jinsi ya kusimamia pesa zao. Nimefurahishwa sana kuona hili NMB mnalitekeleza kwa ufanisi hapa Nanenane," alisema Bashungwa.

Hata hivyo, waziri huyo aliiomba benki hiyo kutoa elimu kama hiyo kwenye vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) ambavyo vimekuwa na matatizo ya ubadhirifu wa fedha za wanachama.

"Niwaombe NMB kuisaidia serikali kutoa elimu hii kwa AMCOS, baadhi yake bado zina matatizo kwenye usimamizi wa fedha. Ingawa serikali tumeendelea kupambana nalo, elimu hii ni muhimu sana kwao," alisema Bashungwa.

Alisema elimu ambayo inatolewa na NMB kwenye maonyesho hayo, ni sehemu ya malengo ya serikali ya kuwainua kiuchumi wakulima, wavuvi na wafugaji ikiwa pamoja na kuzalisha kwa tija.

Kwa upande wake, Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, alisema benki hiyo imetoa Sh. bilioni 161 kwenye mazao ya tumbaku, kahawa na pamba.

Magesse alisema fedha hizo zimepelekwa kwenye mazao hayo kama mkopo na wanufaika wakuu ni wakulima kupitia takribani AMCOS 700.

## PSSSF sasa yaanza kutoa fao la uzazi

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umeanza rasmi kulipa Fao la Uzazi kwa wanachama wake wanawake.

Akizungumza kwenye banda la mfuko huo katika maonyesho ya Nanenane yanayofanyika Viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu, Kaimu Meneja wa PSSSF Mkoa wa Mara, Nyaswi Elias, alisema malipo hayo yameanza ikiwa ni takriban miaka mitatu tangu serikali iunganishe mifuko minne ya hifadhi ya jamii ya PSPF, PPF, LAPF na GEPF na kuzaliwa PSSSF.

Akitaja vigezo vinavyozingatiwa kulipa fao hilo, Elias alibainisha kuwa ni lazima mfaidika awe ni mwanachama mwanamke wa PSSSF, aliyechangia kwa miezi 36, sawa na miaka mitatu na anapaswa kuwasilisha nyaraka zote zinazohitajika kwenye mfuko ndani ya siku 90 baada ya kujifungua.

Akifafanua zaidi kuhusu masharti hayo alisema meneja huyo alisema: "Fao hilo la uzazi mwanachama anaweza kufaidika nalo kwa uzao wa kwanza, wa pili, wa tatu hadi wanne.

"Haijalishi katika moja ya uzao huo kajifungua mtoto mmoja au mapacha au kila uzao kajifungua mapacha, tunachozingatia hapa ni kwamba mwanachama atafaidika na fao hilo mara nne." Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Na. 2 ya Mwaka 2018, ilipitishwa na Bunge ikiunganisha mifuko minne ya pensheni kuunda Mfuko wa PSSSF.Kwa mujibu wa sheria hiyo, mafao ya hifadhi ya jamii ni Pensheni ya Uzeeni, Fao la Ulemavu, Fao la Warithi, Fao la Upotevu wa Ajira, Fao la Ugonjwa, Fao la Uzazi na Mkopo wa Nyumba.

# Unyonyeshaji wachangia utunzaji mazingira

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANAWAKE wanaonyonyesha watoto wametajwa kuwa miongoni mwa watu wanaochangia kutunza mazingira kwa kutonunua maziwa ya dukani ambayo baadaye wanatupa makopo na vifungashio katika maeneo mbalimbali.

Wiki ya Unyonyeshaji kwa mwaka huu inaelezwa kuwa na uhusiano kati ya unyonyeshaji watoto maziwa ya mama na afya bora na kulinda mazingira.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Mkurugenzi wa Shirika linalojihusisha na huduma kwa wazee la Msamaria Mwema, Elisha Mwamkinga, wakati akizungumza na baadhi ya kinamama katika Zahanati ya Mwendapole.

Mwamkinga alisema unyonyeshaji wa watoto maziwa ya mama hupunguza kiwango cha matumizi ya maziwa na vyakula mbadala vya watoto wachanga ambavyo vinakwenda sambamba na matumizi ya vifungashio vya plastiki, nishati kama kuni, mkaa na chupa za kulishia watoto.

Alisema vitu hivyo vyote vinavyotumika katika vyakula mbadala vya watoto, vinachangia ongezeko la hewa inayoathiri mazingira.

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Kibaha, Salma Mohamed, alisema takwimu zimeongezeka kwa watoto wanaonyonyeshwa saa moja baada ya mama kujifungua kutoka asilimia 69 ya mwaka 2016 hadi asilimia 83 mwaka huu.

Aidha, alisema watoto wanaonyonya maziwa ya mama pekee wamefikia asilimia 99.9 kutoka 99 ya mwaka 2016 huku watoto wanaonyonya maziwa mbadala wakipungua kutoka asilimia moja mwaka 2016 hadi asilimia 0.02 mwaka huu.



Mlezi wa Umoja wa Wababa Fedha (UWBF GROUP), Raphael Mindolo, akikata utepe kufungua ofisi ya umoja wao iliyopo Kivule kwa John Fedha, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Agizo la Magufuli kutengeneza 'ambulance' latekelezwa siku 3

**Na Julieth Mkireri,**
PWANI

HATIMAYE Mkoa wa Pwani umetekeleza agizo la Rais Dk. John Magufuli la kufanyia matengenezo ya gari la kubebea wagonjwa katika Wilaya ya Rufiji.

Agizo hilo limetekelezwa zikiwa zimepita siku nne baada ya Rais Magufuli kuongea na wananchi wa wilaya hiyo Julai 30, akiwa njiani kutokea Mtwara na kuelezwa kuwa gari hilo ni bovu halitoi huduma kwa wagonjwa.

Rais Magufuli alitoa maelekezo kwa wilaya hiyo kutatua changamoto ya gari hilo haraka na kufanya kazi ya kuhudumia wagonjwa watakaohitaji huduma hiyo.

Akizungumza mjini Kibaha jana, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, wakati akimkabidhi gari hilo Mganga Mkuu wa mkoa, Gunini Kamba, alisema wametekeleza agizo hilo la Rais.

Mhandiai Ndikilo alisema gari hilo lilipelekwa kwa Wakala wa Huduma za Umeme na Ufundi (TEMESA) kwa ajili ya matengenezo na limekamilika tayari kwa kwenda kufanya kazi za kubeba wagonjwa.

"Tulitakiwa tutekeleze agizo ndani ya siku tano, lakini sisi siku moja kabla tumefanikiwa kukamilisha matengenezo na sasa namkabidhi Mganga Mkuu wa mkoa litapelekwa Rufiji," alisema Ndikilo.

Aliwataka waganga wakuu wa wilaya za mkoa huo kuhakikisha magari ya wagonjwa yanafanya kazi na kama kuna tatizo lirekebishwe mapema wasisubiri kukumbushwa wajibu wao na viongozi wakuu.

Alisema kuwa viongozi wote walio ndani ya mkoa watatue matatizo kabla viongozi wa ngazi za juu hawajafika na kuwakumbusha wakati yako ndani ya uwezo wao.

Katika hatua nyingine alisema kuwa tayari ujenzi wa vyoo saba na mabafu mawili unaendelea kwa ajili ya soko la Wilaya ya Kibiti na umefikia zaidi ya asilimia 65 hadi Jumamosi ni upauaji.

Alisema kuwa vyoo vyote saba na mabafu mawili vitakuwa vimekamilika kwa asilimia 100 Jumamosi Agosti 8, na kuanza kutumika kwa kuwa hatua ya kupaua na kuezeka itakuwa imekwisha na mifumo ya maji na

# Waziri akoshwa utendaji wa WCF

**Na Mwandishi Wetu,**
BARIADI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, ameupongeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kutokana na huduma ambazo umekuwa ukitoa kwa wafanyakazi walioumia, kuugua au kufariki dunia kutokana na kazi.

Kairuki alitoa pongezi hizo jana alipotembelea banda la mfuko huo kwenye maonyesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa katika Viwanja vya Nyakabindi nje kidogo mwa mji wa Bariadi mkoani Simiyu.

Waziri huyo alitoa pongezi hizo baada ya kupata maelezo ya shughuli za mfuko kutoka Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa WCF, Sebera Fulgence, Kairuki akikiri kuvutiwa na majibu ya namna fidia inavyolipwa kwa mfanyakazi aliyeumia au kufariki dunia kutokana na kazi.

"Mwisho wa siku mtu amepata ulemavu wa kudumu angalau consolation (faraja) anayopata ni kuona wanawe wanaendelea vizuri au kama amefariki dunia walau fidia isaidie watoto na mjane pia.

"Lengo la serikali ni kutoa msaada wa uhakika. Ninawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayofanya," alisifu Waziri Kairuki ambaye alikuwa amefuatana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga.

Mfuko huo unashiriki katika maonyesho hayo ili kukutana na wadau wote na wananchi kwa ujumla wakiwamo wafanyakazi kutoka sekta ya umma na binafsi.

Kauli mbiu ya mwaka huu ya maonyesho hayo yanayofanyika mkoani Simiyu kwa mwaka wa tatu mfululizo ni 'Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Chagua Viongozi Bora 2020'.

# Bosi SBL achaguliwa mjumbe wa CEOrt

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti, amechaguliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Jukwaa la Maofisa Watendaji Wakuu Tanzania (CEOrt).

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na CEOrt, ilieleza kuwa, Mark pamoja na David Nchimbi, anayefanya kazi na kampuni ya Deloitte, walichaguliwa kuwa wajumbe wa bodi ya jukwaa hilo katika mkutano uliofanyika mwisho mwa wiki.

Mark ana Shahada ya takwimu kutoka Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda, Shahada ya Uzamili ya Biashara kutoka Shule ya Biashara ya London pamoja na Shahada ya Uzamili ya Utawala kutoka Chuo Kikuu cha Edinburg nchini Uingereza.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Mark alisema: "Ninafurahi kuwa mjumbe wa bodi ya jukwaa hili muhimu haswa katika kipindi hiki ambacho dunia inapitia kipindi kigumu. Jukwaa hili ni kiungo muhimu kati ya sekta binafsi na sekta ya umma na nitatumia uwezo na maarifa yangu kwa ajili ya kuhakikisha sekta binafsi inaendelea kuwa kichocheo muhimu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi,"

Mwenyekiti wa jukwaa hilo, Sanjay Rughani, alisema CEOrt inawakaribisha Mark na David na kuongeza kuwa uzoefu wao wa uongozi wa zaidi ya miongo kadhaa utaliwezesha jukwaa hilo kutekeleza mipango yake.

"Nimewafahamu Mark na David kwa miaka kadhaa na ni matarajio yangu kuwa tutafanya kazi kwa ukaribu zaidi katika masuala mbali mbali yanayohusisha majadiliano na Serikali, wadau wa maendeleo, viongozi wa sekta binafsi kwa ajili ya kusukuma mbele gurudumu la maendele ya kijamii na ya kiuchumi," alisema.

# Watakiwa kutumia fursa za mipakani

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

WAFANYABIASHARA na wamiliki wa viwanda mkoani Kagera wameshauriwa kutumia fursa ya kupakana na nchi nyingi kutafuta masoko ya ndani na nje ya kwa ajili ya kuuza bidhaa wanazozalisha ikiwamo kahawa.

Akizindua maonyesho ya Nanenane katika viwanja vya Kyakailabwa, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawilo, alisema serikali inajitahidi kuweka mazingira bora ya kufanyia biashara ikiwamo kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa kutosha na uwepo wa miundombinu bora kama barabara.

"Lengo la serikali kufanya yote haya ni kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji, wanachopaswa kufanya wafanyabiashara ni kuonyesha ushirikiano kwa serikali na kupambana kutafuta masoko badala ya kulalamika tu" alisema Kinawilo.

Alisema Mkoa wa Kagera unapakana na Rwanda, Burundi na Uganda, na kupitia njia ya maji (Ziwa Victoria) inapakana na Kenya, lakini akadai kuwa pia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Sudan haziko mbali , na kwamba katika mataifa hayo yapo masoko ya kutosha kuuza bidhaa wanazozalisha.

# Serikali yawawezesha wakulima kupata tril. 2.7/-

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

WIZARA ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Bodi ya Mazao nchini, imefanikiwa kuwawezesha wakulima wanaouza mazao mbalimbali kupata jumla ya Sh. trilioni 2.7 katika kipindi cha mwaka 2020 na kuwafanya wakulima hao kuondokana na hali ya umaskini.

Akizungumza katika siku ya kuhamasisha ushirika iliyofanyika katika Kijiji cha Ushirika kwenye Maonyesho ya Wakulima katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema kiasi hicho cha fedha kilitokana na kuuzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, ambao serikali imekuwa ikihamasisha. Aliyataja mazao yaliyouzwa kupitia ushirika ni ya ufuta, choroko, dengu, mkonge, pamba, maziwa, chai, korosho, zabibu, kahawa na tumbaku.

Aliongeza kuwa kupitia mfumo huo, umewezesha pia wanunuzi kupata mazao yenye ubora.

Waziri Hasunga alisema licha ya sekta ya ushirika kutoa mchango katika kilimo, lakini imeweza kusaidia kutoa ajira kwa wananchi ambapo hadi kufikia Desemba 2019 wananchi zaidi ya 9090 waliweza kupata ajira zikiwamo za kudumu, mikataba na za msimu ukilinganisha na ajira 32,668 za Desemba 2018.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, alisema kupitia vyama vya ushirika, wananchi hasa wa kipato cha chini wengi wao wakiwa wakulima kwa pamoja wameweza kupatiwa mikopo yenye thamani ya Sh. trilioni 1.3 hadi kufikia Aprili 2020. Dk. Ndiega, alisema kuwa hatua hiyo ya utoaji wa mikopo kwa wakulima imewafanya kushika nafasi ya tatu baada ya Benki za NMB na CRDB huku wakulima wakiinukia kiuchumi kwa kutumia mikopo hiyo kwa ajili ya uzalishaji mali ikiwamo kilimo na biashara.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, akizungumza kwenye siku ya ushirika, alisema ni wazi maendeleo ya uhai wa ushirika unategemea wakulima, wafugaji na wavuvi kujiunga na vyama vya ushirika vyenye viongozi bora.

Waziri Kairuki alisema dhamira ya serikali ni kuona vyama vya ushirika vinashiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa Taifa wa maendeleo wa miaka mitano ikiwamo ufufuaji wa viwanda vinavyotokana na ushirika.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Angellah Kairuki (wa tatu kulia) na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa pili kulia), wakipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Tigo Kanda ya Ziwa, Gwamaka Mwakilembo (mwenye miwani), walipotembelea banda la Tigo, katika maonyesho ya Nanenane mkoani Simiyu juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lukuvi atekeleza maagizo ya JPM

**Na Mary Geofrey,** MKURANGA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametekeleza agizo la Rais John Magufuli la kurejesha serikalini ekari 4,222 ili kupimwa na kugawiwa kwa wananchi na nyingine kuendelezwa.

Lukuvi alitekeleza agizo hilo jana wilayani Mkuranga mkoani Pwani, ikiwa ni siku chache baada ya Rais Magufuli kupokea malalamiko ya wakazi hao wakidai maeneo yao kuvamiwa na wawekezaji.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kazole, Lukuvi aliagiza Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kuchukua ekari 750 kati ya 1,750 zinazomilikiwa na mwekezaji Soap and Allied Industries, ili kuzipima na kuwagawia wananchi wa eneo hilo.

Aliagiza ekari nyingine 1,000 zipimwe na kupangiwa kwa mwekezaji huo ambaye ataeleza aina ya uwekezaji anaofanya na kati ya eneo hilo, halmashuari pia itatumia kwa ajili ya huduma za jamii.

"Rais Magufuliameniagiza kuja hapa, nimefuatilia kwa kina kuhusu mgogoro huu uliodumu kwa zaidi ya miaka 30, haiwezekani mwekezaji akamiliki ekari 1,750 kwa miaka yote hii, lakini ameendeleza asilimia 60 tu, eneo lingine amelitelekeza, tena ni la wananchi," alisema Lukuvi.

Aliagiza maeneo hayo kupimwa na halmashauri kwa ajili ya kuyapima na kuyarasimisha kwa wakazi wa vijiji vyote na maeneo mengine kupangiwa matumizi kwa mujibu wa sheria.

Sambamba na hilo, alisema eneo lingine ni la ekari 2,472 liloko eneo la Luzando wilayani hapa, linalomilikiwa na mwekezaji ambaye ni Emtiyaz Ahmed Rajwan na Karim Ahmed Manji, sehemu kubwa ni shamba ambalo liko ndani ya vijiji vinne ambavyo tayari vilishapimwa ambavyo ni Luzando, Mwanambaya, Mlaleni na Mipeko.

Alisema wakati wawekezaji hao wakinunua shamba hilo, sehemu kubwa ilikuwa ikimilikiwa na wanakijiji na hivyo tayari wawekezaji hao walikuwa wameshatengewa na kumiliki ekari 1,000 tu kati ya ekari 2,472 walizomilikishwa awali.

Lukuvi alisema hati ya shamba hilo pia imewekwa rehani kwa mkopo wa Benki ya CRDB kwa kiwango ambacho hakikutajwa.

"Ninaagiza eneo hili lirudi kwa halmashauri kwa ajili ya kupimwa na kurasimishwa kwa wananchi wa vijiji hivi vinne na mwekezaji aturejeshee hati yetu na ameshakubali kufanya hivyo," alisisitiza Lukuvi.

## NMB yajivunia mapinduzi kilimo cha pamba

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

BENKI ya NMB imesema ni mshiriki muhimu katika mchakato wa kuleta mabadiliko chanya kwenye kilimo cha pamba mkoani Simiyu kwa kuchangia kikamilifu utekelezaji wake kupitia njia mbalimbali ikiwamo ukopeshaji wadau wote kwenye mnyororo wa thamani wa zao hilo.

Imesema mchango wa NMB katika mkakati maalum wa miaka mitano wa mapinduzi ya kilimo cha pamba mkoani humo pia unahusisha utoaji elimu kwa wakulima na vyama vyao vya ushirika (AMCOS) na kuwasaidia kujiunga na mfumo rasmi wa kifedha nchini.

Akizungumza katika banda la mkoa kwenye viwanja vya Nanenane lilipotembelewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwezeshaji), Angela Kairuki, jana, Meneja wa Kanda ya Magharibi wa benki hiyo, Sospeter Magese, alisema pia wamesaidia kuziunganisha AMCOS 26 ambazo zinashiriki kwenye programu hiyo maalum.

Banda hilo lipo kimkakati kuonyesha nini kinafanyika kwenye utekelezaji wa Mkakati Maalum wa Miaka Mitano (2019-2024) wa Mapinduzi ya Kilimo cha Pamba mkoani Simiyu ambao ulizinduliwa rasmi mwezi Machi mwaka jana. Lengo lake kubwa ni kukiendeleza na kukiongezea thamani kilimo cha pamba ambacho ndiyo shughuli kubwa ya kiuchumi mkoani Simiyu kwa kutatua changamoto za maendeleo yake ikiwamo ile ya upatikanaji mitaji na masoko.

Kwa mujibu wa Magese ambaye ni Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, moja ya ushiriki wao mkubwa katika mkakati huo ni kutoa Sh. bilioni 1.9 kwa ajili ya kukarabati maghala ya pamba kwa lengo la kuhakikisha zao hilo linahifadhiwa kisasa na kwa usalama zaidi.

"Sisi tunashiriki kikamilifu katika programu hii na tayari tumetoa kiwango cha Sh. bilioni 1.9 kukarabati maghala ambayo kwa muda mrefu sana yalikuwa yamechakaa ili zao letu la pamba linapovunwa kule mashambani liweze kuhifadhiwa vizuri," Magese alimweleza Kairuki.

Pia alisema NMB imesaidia kufungua akaunti 86,000 za wakulima wa pamba ingawa kunachangamoto ya matumizi yake kutokana na wanunuzi wengi wa zao hilo kufanya malipo kwa fedha taslimu.

Benki hiyo imependekeza na kumwomba waziri kuhakikisha utaratibu huo unabadilishwa, jambo ambalo serikali imelikubali na kuamuru kwamba kuanzia sasa malipo yote ya mauzo ya pamba yafanyike kupitia akaunti za benki.

ama

ALHAMISI AGOSTI 6, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Utekelezaji maagizo ya vita corona bado tatizo shuleni**



Ukurasa 13

HII HAPA SHIDA YA KUVIMBA KOO 'TONSILS', INAVYOTIBIWA



Ukurasa 14

**Mjamzito, mnyonyeshaji na safari inayowatetea kwa mlo, afya mwili**

AFYA

# Waganga jadi wawekwa 'kitimoto' kisa kuendekeza ramli chonganishi

## • RPC: Watumaji, wanaotumwa tunao!

**Na Marco Maduhu, Shinyanga**

MKOA wa Shinyanga awali ulikabiliwa na adha ya ugumu wa mauaji ya wazee yatokanayo na imani za kishirikina, kwa kila aliyekuwa na macho mekundu alihisiwa uchawi, baadhi wakiangukia kukatwa mapanga.

Chanzo kikuu kinatajwa ni imani za kishirikina, yanayosababishwa na waganga wa jadi, kupitia ramli wanazopiga kuwaambia wateja wao kuwa wamerogwa na wazee, ndipo mchakato wa kuanza kutekelezwa mauaji ya kilipiza kisasi yanapoanzia.

Namna ya kuyatekeleza, huwa kuna watu maalumu wanaokodiwa kufanya mauaji kazio hiyo, ikidaiwa wanapewa ujira wa fedha kuanzia Sh. 300,000.

NENO LA RPC

Mwaka jana, Polisi mkoani Shinyanga liliwakamata waganga wa jadi 19 wapiga ramli, wakiwa na nyara za serikali wanazotumia kama vile mikia ya nyumbu, ngozi za kenge na simba, kucha za simba, mayai ya mbuni, kichwa cha kenge, jino la ngiri, na bundi mmoja.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Debora Magiligimba, anasema ukamataji wa waganga hao wa jadi, ni uamuzi muhimu katika kukomesha matukio ya mauaji dhidi ya wazee.

"Mauaji ya wazee yatokanayo na imani za kishirikina mkoani Shinyanga yamepungua kwa kiasi kikubwa, ikilinganisha na miaka ya nyuma. Hali hii inatokana na kuwakamata waganga wa jadi ambao hupiga ramli chonganishi, sababu wao ndio chanzo kikubwa cha mauaji haya,"anasema Kamanda Debora.



Kamanda wa Polisi Mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa wazee, kujadili athari za imani potofu za kishirikina na ramli chonganishi. **PICHA: MARCO MADUHU.**

"Januari mwaka huu (2020), tulifanikiwa kumkamata mganga maarufu wa upigaji ramli chonganishi," anasema, huku akifafanua la hatua hiyo iliendana na kuwanasa watu wanne waliokodiwa kutekeleza mauaji hayo hayo mwaka huu.

Kwa mujibu wa Kamanda Debora, watu hao wanadaiwa kukodishwa kufanya kazi hiyo kwa ujira wa Sh. milioni tatu.

Aidha, anasema mauaji saba yalitokea mwaka jana kati ya Januari na Juni na mwaka huu idadi imeshuka kwa kipindi kama hicho, ameuawa mzee mmoja.

**BARAZA LA WAZEE**

Laurent Mihayo, Mjumbe wa Baraza la Wazee Wilayani Kahama, Shinyanga, katika taarifa anayotoa kwa niaba ya Katibu wa Baraza hilo, anasema waganga wa jadi wapiga ramli wamekuwa tatizo katika ukomeshaji mauaji ya wazee, unaosukumwa na ushirikina.

"Takwimu za mwaka jana zinaonyesha kulitokea mauaji ya wazee wawili yatokanayo na imani za kishirikina, lakini mwaka huu hadi sasa tunamshukuru Mungu hakuna," anaongeza Underson Lyimo, Katibu wa Baraza Wazee Mkoa.

Pia, Katibu wa Baraza la Wazee ngazi ya Wilaya Shinyanga, Ngassa Maganga, anasema, pia elimu inapaswa kutolewa kwa umma ubadilike dhidi ya nyendo za ramli za kishirikina zinazoangukia kuwashuku wazee.

Anaainisha undani wa wazee kuwa na macho mekundu na hasa wanawake, sababu kuu ni kupika kwa kutumia kuni kwa muda mrefu na daima haihusiani na dhana ya kuhusika na uchawi.

**WANAOWATETEA WAZEE**

Mratibu wa Shirika la Tawlae, Eliasenya Nnko linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga, ambao wanatekeleza mradi wa kuifanya mifumo ya utawala kuwajibika kwa wazee ikiwamo kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili, yakiwamo masuala ya afya, pamoja na kutokomeza mauaji ya wazee.

Anasema tangu mradi huo uanze kufanya kazi mkoani Shinyanga mwaka 2018, wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la mauaji ya wazee tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma. Mradi huo unakoma mwezi huu.

"Vitu ambavyo tunavifanya kwenye mradi wetu huu, nikutoa elimu ya ukatili dhidi ya mauaji ya wazee kwa kukutana na wazee wenyewe, waganga wa jadi, wazee maarufu, viongozi wa dini, maofisa ustawi, wakuu wa wilaya na jeshi la Polisi,"anasema Nnko, anayekiri kushuhudiwa mafanikio.

"Sisi kama Shirika la Tawlae linatotetea haki za wazee, tunaipongeza serikali na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kupambana na hawa waganga wa jadi wanaopiga ramli chonganishi na kufanikiwa kupunguza matukio ya mauaji ya wazee," anaongeza.

Aidha, anataja jicho la kitaifa upande wa serikali, unaonuia kutokomeza mauaji ya wazee, ufikapo mwaka 2023.

AFYA

JICHO LA SIMIYU

# Utekelezaji maagizo ya vita corona bado tatizo shuleni

## • Walimu: Hali halisi inatuelemea
## • Shida kuu ni kunawa na barakoa
## • Elimu 'corona ni nini' imefanikiwa



Ndivyo ilivyo uhalisia wa baadhi ya wanafunzi wa Bariadi, wanavyojihami na janga la corona kwa nyenzo za maji tiririka na sabuni. **PICHA ZOTE: HAPPY SEVERINE**

**Na Happy Severine, BARIADI**

JUNI 29 mwaka huu, serikali ilitangaza kufunguliwa shule na vyuo nchi nzima, baada ya kufungwa kwa miezi mitatu, kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu, inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19).

Serikali ilitoa tahadhari kuwa bado ugonjwa huo upo na lazima taasisi zote shule na vyuo vya elimu vifuate masharti yanatolewa na wataalamu wa afya, kujikinga na ugonjwa huo.

Pia, kabla vyuo na shule kufunguliwa, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, zilitoa miongozo ya namna ya kujikimu kiafya.

Baadhi zilihusu hatua zitakazotakiwa kuchukuliwa na asasi hizo za kielimu, kama tahadhari ya kujikinga kuenea au kupata ugonjwa huo.

Waziri anayehusika na Afya, Ummy Mwalimu, katika mwongozo wa kwanza Mei, 27, 2020, alielekeza zaidi ya hatua 10 zinazotakiwa kuchukuliwa za tahadhari dhidi ya corona.

Hapo kuna suala la kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kila wakati, wanafunzi na walimu kuvaa barakoa, kuepuka msongamano na kutolewa elimu kwa wanafunzi na walimu, jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo.

Baadhi ya shule zimeweza kutekeleza maagizo hayo kwa kiwango kikubwa na kuna zingine nyingi zinazoshindwa kufanikisha utekelezaji wa kanuni hizo na hasa zilizoko vijijini.

**"Mfano darasa la tano wapo wanafunzi zaidi ya 200 na wanakaa chumba kimoja. Kwa maagizo ya serikali, lazima wavae barakoa, sasa katika kuhakikisha wote wanavaa, inakuwa ngumu wengine utakuta wamevua, wanabadilishana na kuzichezea," anaeleza Mwalimu Yamungu.**

Nipashe ilitembelea baadhi ya shule katika mkoa wa Simiyu, kutathmini uhalisia uliopo.

Miongoni mwa vigezo vilivyozingatiwa katika ukaguzi huo ni pamoja na unawaji mikono kila mara kwa sabuni na maji tiririka, uvaaji barakoa na ukaaji umbali wa mita moja kati ya mtu na mwingine.

Mengine yanatajwa ni kufuatilia kutekelezwa kanuni zinazoonekana na kuwa vikwazo kuvitekeleza kwa shule nyingi.

**UVAAJI BARAKOA**

Maelekezo ya Wizara ya Afya, inazitaka wizara zinazohusika na elimu kuhakikisha zinatoa maelekezo kwa shule na vyuo, walimu na wanafunzi wanavaa barakoa wakiwa kwenye msongamano, isipokuwa wakati wa mapumziko.

Ni kanuni inayoonekana kushindwa kutekelezeka katika baadhi ya shule na hasa zilizopo vijijini, kwa walimu hata kwa wanafunzi, changamoto imegundulika ni upatikanaji wake, pia uwezo wa kuzinunua.

Katika Shule ya Msingi Mahaha iliyoko Halmashauri ya Mji Bariadi, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Charles Yamungu, anasema mbali na upatikanaji wake kuwa mgumu, pia ufuatiliaji kuhakikisha wanafunzi wanavaa barako kila wakati, imekuwa ni ngumu.

"Kama ambavyo tunawajua wanafunzi kuwasimamia kuna kazi ngumu kweli, hasa wale wadogo, ukizingatia ni wengi. Lakini unahitaji muda kuwafuatilia mara kwa mara, kuhakikisha muda wote wawe wamevaa," anasema Yamungu.

Mwalimu Mkuu huyo anasema, kutokana na mazingira ya shule na wanafunzi kujazana kwenye chumba kimoja kwa sababu ya ukosefu wa madarasa ya kutosha, kunakuwapo msongamano, hali inayotoa umuhimu kwa maagizo ya wataalamu wa afya kuhusu uvaaji barakoa.

"Mfano darasa la tano wapo wanafunzi zaidi ya 200 na wanakaa chumba kimoja. Kwa maagizo ya serikali, lazima wavae barakoa, sasa katika kuhakikisha wote wanavaa, inakuwa ngumu wengine utakuta wamevua, wanabadilishana na kuzichezea," anaeleza Mwalimu Yamungu.

Hata hivyo, walimu wanasema tatizo linajitokeza zaidi katika kuwafuatilia wanafunzi kuhakikisha wanavaa barakoa, pindi wanapokusanyika hata darasani, kwani wengi huzichezea, kuchangiana au hata kuibiana.

**KUNAWA MIKONO**

Maagizo ya kiafya kutoka serikalini ni kwamba, shule na chuo kuhakikisha wanafunzi wao wananawa mikono kwa sabuni kwa maji tiririka kabla ya kuingia darasani, kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo.

Ni kanuni inayoonekana kuwa ngumu kuitekeleza katika shule za msingi vijijini, huku za mjini zinajitahidi, kwa sababu ya mazingira bora walio nayo.

Adalbert Chambia, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Gamondo 'A' anasema shida kuu kwao ni upatikanaji majisafi, kwa sababu hawana huduma nzuri.

"Huku asilimia kubwa maji ambayo yanapatikana ni yale ambayo yapo kwenye madimbwi, ambayo siyo safi.

"Ukitaka kupata safi, lazima kuchimba kwenye mto ambao uko umbali wa kilomita tano kutoka hapa shuleni," anaeleza Mwalimu Chambia, huku akitaja idadi ya wanafunzi wote shuleni ni zaidi ya 2000.

"Ukiangalia hapa wanafunzi walivyo wengi utaona tabu ambayo tunaipata. Pia, wanafunzi kuwasimamia ili watumie vizuri maji, nalo ni tatizo maana ni wengi, ingawa sabuni ipo ya kutosha na tumenunua matanki ya kutosha," anasema.

Mwendesha bodaboda akiwa kwenye kituo chake cha biashara.

**SHULE MIJINI**

Katika Shule ya Msingi Kidinda, iliyoko katikati ya mji Bariadi, wanalalamika shida yao ni upatikanaji maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Mazingira Bariadi (BARUWASA).

Mwalimu Mkuu, Robert Mathias, anasema hawana shida ya maji, bali tatizo lao ni namna ya kuwasimamia wanafunzi kuhakikisha wananawa mikono kila wakati, pindi wanapotaka kuingia darasani.

"Wanafunzi hapa ni wengi sana, kuwasimamia kila wakati wanawe mikono ni kazi ngumu, ingawa tunawaelimisha kila wakati. Wengi wao wanafuata maelekezo, ila baadhi wale wadogo wanajisahau," anaeleza.

**MSONGAMANO**

Suala la wanafunzi kukaa mita moja kati ya mmoja na mwingine utekelezaji wake unadaiwa kuwa mgumu kwa shule zote za msingi, mjini na vijijini.

Hapo Nipashe imebaini shida kuu ni idadi kubwa ya wanafunzi kuzidi uwezo wa vyumba vya madarasa na madawati yake.

Katika Shule ya Msingi Gamondo 'A' yenye wanafunzi 2,505 inahitaji madawati 835 na vyumba vya madarasa 56, ili kukidhi kanuni hiyo ya kukaa umbali wa mita moja kati mwanafunzi na mwingine.

Mwalimu Mkuu Chambia, anasema shule ina vyumba vya madarasa 17 ikiwa na madawati 719, hivyo wanafunzi wanakaa kwa kubanana na kwenye dawati moja wamejaribu kupunguza idadi ya wanafunzi wanakaa watatu.

Anaendelea: "Zamani wanafunzi walikuwa wakikaa wanne hadi watano kwenye dawati moja ambalo uwezo wake ni wanafunzi wawili, kwa sasa baada ya hali hii, tumejaribu kupunguza wanakaa watatu, lakini bado."

**ELIMU YA CORONA**

Utolewaji elimu kila mara kuhusu namna ya kujikinga na ugonjwa huo na madhara yake kwa wanafunzi, Nipashe imegundua kwa kiwango kikubwa inatelezwa, walimu wamekuwa wakitumia wastani wa dakika 10 kabla ya kufundisha, kuelimisha jambo hilo.

"Kabla ya shule kufunguliwa walimu tulipewa elimu ya ugonjwa huu na jinsi gani tutaweza kuwafundisha wanafunzi na tumekuwa tukiwaelimisha mara kwa mara kabla ya kuanza kupindi," anaeleza Mwalimu Mukama Mukama.

AFYA

# HII HAPA SHIDA YA UVIMBAJI KOO 'TONSILS', INAVYOTIBIWA

## • Yawanasa watoto hadi miaka 25

**Na Jackson Paul**

UNAIJUA 'tonsiltis'? Ni hali ya kuvimba tezi za kooni ambazo katika utaalamu wa kawaida inatamkwa 'tonsils.' Hiyo ni mishipa yenye mwonekano wa umbo kama yai na hukaa pande mbili nyuma ya koo.


Mara nyingi kuvimba tezi huko kunasababishwa na uvamizi wa virusi au bakteria. Matibabu yake sahihi yanategemea chanzo cha tatizo, yaani iwapo ni kwa bakteria au virusi. Ni muhimu mtu akapimwa kujua chanzo halisi, kabla hajapatiwa matibabu stahiki.

Kuna wakati upasuaji unafanyika kuondoa kabisa matezi, lakini unafanyika tu pale anapopendekeza daktari na mara nyingi inakuwa pake tatizo linajirudia kila mara.

Pia, katika namna tatizo linaposhindwa kupona kwa kutumia dawa za kawaida au tezi linaposababisha matatizo mengine makubwa mwilini.



Shida ya ugonjwa tonsils na matibau yake. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**




### DALILI ZAKE

Kuvimba kwa tezi mara nyingi inawaathiri zaidi watoto wenye umri mdogo (ambao hawajaanza shule) na walio katika ujana umri unaokaribia utu uzima (miaka 15-25).

Dalili anazopata ni pale 'tonsilitis' zinakuwa nyingi, zikiwa na sifa ya kuvimba tezi, kuwa na rangi nyekundu; kuhisi maumivu wakati wa kumeza chakula au kushindwa kumeza chakula.

Mengine inatajwa kuwa ni maumivu ya koo, utando mweupe au wa njano sehemu ya matezi, kupata homa, kukua kwa vitoki 'lymph nodes' eneo la shingo na sauti kukwaruza.

Pia, kuna suala la mtu kutokwa harufu mbaya mdomoni wakati wa kupumua, shingo kukakamaa na maumivu ya kichwa.

Kwa watoto wadogo wasio na uwezo wa kueleza hisia zao au hali wanayojisikia, huweza kuonekana wakiwa na dalili kama kutokwa na mate 'udenda' bila ta kujizuia, kukataa au kugoma kula, pamoja na kukasirika kila mara pasipo sababu yoyote.

Mara nyingi 'tonsillitis' inasababishwa na uvamizi wa virusi, japokuwa uvamizi wa bakteria pia unaweza kusababisha tatizo hilo. Bakteria ambaye mara nyingi husababisha 'tonsillitis' na maumivu ya koo anajulikana kama Streptococcus pyogenes.

### KUSHAMBULIWA TEZI

Kwa kawaida tezi (tonsils) ni sehemu ya kwanza ya kinga 'ulinzi' wa mwili dhidi ya bakteria au virusi wanaoingioa mwilini kwa njia ya kinywa.

Kutokana na tezi kuwapo katika eneo hilo la kinywa, huangukia hatari ya kupata madhara ya kila mara.

Hata hivyo, kazi ya kulinda mwili inayofanywa na tezi za kooni hupungua kadri mtu anapoingia katika utu uzima na inatajwa kuwa sababu inayochangia kupungua madhara.

Nafuu kwa watu wazima iko juu, tofauti na watoto wadogo ambao tezi zao hutumika zaidi kwa ajili ya ulinzi wa mwili.

Zipo hali mbalimbali zinazosababisha mtu kuwa hatarini kupata tatizo hilo la tonsils.

Pia, anaeleza tatizo linawaangukia zaidi watoto na mara chache kwa wenye umri chini ya miaka miwili.

Kwao watoto wenye umri kati ya miaka mitano hadi 15, hupata tatizo hilo kutokana na mashambulizi ya bakteria na ile inayosababishwa na virusi, huwapata zaidi wenye umri chini ya miaka mItano.

### VIJIDUDU NA BAKTERIA

Mara nyingi watoto wadogo waliopo shule hugusana na wenzao, hali inayowawekea hatari kubwa ya maambukizi. Lakini, watoto mara nyingi huweza kugusana na vitu hatari vyenye vijidudu na kupata matatizo.

Madhara yanatokea kwenye tonsils, pale mtu anapopatwa na matatizo, hasa mazingira yanapokuwa sugu.

Ni madhara yanayojumuisha kupumua kwa shida hasa anapokuwa usingizini, kusambaa kwa maambukizi pembezoni mwa tezi (tonsillar cellulitis) na maambukizi yanayochangia kukusanyika usaha nyuma ya tezi 'peritonsillar abscess'.

### MATIBABU TEZI

Katika kutibu tatizo uvimbe wa tezi, zipo aina tatu za matibabu zinazotumiwa, yaani; utumiaji wa dawa, matibabu ya kufanyika nyumbani bila kutumia dawa na matibabu kwa njia ya upasuaji.

Iwapo tatizo la kuvimba kwa tezi ama limesababishwa na virusi au bakteria, kuna njia zinazoweza kufanyika nyumbani na kusaidia kumfanya mgonjwa kupata nafuu, akajihisi vizuri kiafya.

Iwapo chanzo cha kuvimba tezi kimebainika ni virusi, basi matibabu ya nyumbani huwa ndio sahihi zaidi na daktari hatakupangia dawa za bakteria (antibiotics).

Mara nyingi kwa njia hii ya matibabu ya nyumbani mtoto huweza kupata nafuu au kupona baada ya muda wa siku saba hadi kumi.

Njia zinazoweza kutumika nyumbani pale chanzo cha kuvimba tezi kimebainika kuwa ni virusi, hatua zifuatazo:

Kupumzika; iwapo mgonjwa ni mtoto, mzazi anapaswa kumshawishi apate muda wa kulala vizuri.

Kunywa maji ya kutosha yanayompatia mwana maji ya kila mara, ili kusaidia kuzuia koo lisiwe kavu, hata akajihisi vibaya.

Kusukutua kwa kutumia maji yenye chumvi, kunapaswa kufanyika kwa kuandaa maji yaliyochanganywa na chumvi, walau kijiko kimoja cha chai kwa glasi moja ya maji ya vuguvugu, kisha sukutua maji hayo kwa muda mfupi na kutema. Hiyo inasaidia sana kuleta nafuu kwa mgonjwa.

Kutibu maumivu na homa; mgonjwa anapaswa kujadili na daktari kuhusu utumiaji dawa za kupunguza maumivu, ili kusaidia kumaliza maumivu ya koo au kudhibiti homa.

Hata hivyo, homa ndogo zisizoambatana na maumivu ya koo hazihitaji matibabu yoyote.

### MATUMIZI DAWA

Iwapo kuvimba tezi kumesababishwa na bakteria, daktari humpangia mgonjwa dawa za antibaiotiki na iliyozoeleka ni aina ya penicillin. Wapo watoto wenye aleji ya dawa hizo na daktari anampangia mgonjwa dawa nyingine tofauti.

Hata hivyo, ni muhimu kwa mgonjwa kumaliza dozi hata kama dalili za zimeshatokomea. Kushindwa kumaliza dozi kunatajwa kusababisha tatizo kubwa zaidi, bakteria kusambaa na kuvamia sehemu nyingi mwilini.

Kusambaa bakteria, kunaweza kumsababishia mtoto hatari kubwa ya tatizo la kuvimba figo, ijulikanayo kitaalamu 'kidney inflammation.'

### TIBA UPASUAJI

Inaelezwa kwamba, iwapo mtu anaandamwa na tatizo la kujirudia kuvimba tezi au dawa za kutibu bakteria kushindwa kufanya kazi vizuri kwa mgonjwa, basi upasuaji wa kuondoa kabisa tezi 'tonsillectomy' huweza kuwa njia bora zaidi la kumaliza tatizo.

Kuna vigezo kadhaa hufikiwa na unahitaji, hata upasuaji kwa mwenye shida ya koo kufanyika. Mosi, ni mtu anapopata tatizo la kuvimba tezi zaidi ya mara saba katika kipindi cha mwaka mmoja.

Pili, ni pale kuvimba tezi kunamsababishia mgonjwa kuziba njia ya hewa na mtu anashindwa kupumua vizuri anapokuwa amelala.

Tatu, iwapo mgonjwa anapata tatizo kubwa la kumeza chakula na nne, mgonjwa anapata usaha kwenye sehemu ya tezi ambao hauonyeshi dalili ya kupona, hata pale mtu anapotumia dawa za antibakteria.

### KUIZUIA 'TONSILS'

Virusi na bakteria vinavyosababisha tatizo la kuvimba tezi, huambukizwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda mwingine. Kwa maana hiyo, njia bora ya kuzuia ni kuiweka katika hali ya usafi kila wakati.

Mzazi, anapaswa kumfundisha mwanawe mambo yafuatayo:

Kunawa mikono mara kwa mara, haswa baada ya kutoka chooni na kabla ya kula.

Kuepuka kushirikiana chakula, glasi za kunywea maji, chupa za maji au vyombo vingine vya kulia chakula.

***Mwandishi anapatikana kwa barua pepe: jacpole@gmail.com***

AFYA

WIKI YA UNYOYESHAJI

# Mjamzito, mnyonyeshaji na safari inayowatetea kwa mlo, afya mwili

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KILA Agosti Mosi hadi 7 ya mwaka, Tanzania huungana na nchi nyingine duniani, kuadhimisha wiki ya unyonyeshaji, inayolenga kukumbusha jamii vitu muhimu katika unyonyeshaji maziwa ya mama.

Maziwa ya mama yanatajwa kitaalamu kuwa ni muhimu kwa afya na makuzi ya mtoto, licha ya umuhimu huo, bado kunatajwa kasoro katika unyonyeshaji, ikiwamo kuzingatia lishe bora.

Hata hivyo, suala la ulaji vyakula bora kwa mjamzito na mama anayenyonyesha imekuwa tatizo kwa jamii, hali inayowasababisha watoto kukosa virutubisho muhimu kwenye ukuaji na kinga asilia dhidi ya maradhi.

Takwimu za mwaka wa fedha 2015/2016 (TDHS) na zingine 2018 (TNNS) zinaonyesha asilimia 43 ya watoto nchini wanayonyeshwa hadi kufikia umri miaka miwili.

Takwimu zilizotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), zinaonyesha takribani watoto milioni 7.6 duniani hawanyonyeshwi kila mwaka.



Mama akimnyonyesha mwanawe.

### OFISA LISHE

Ofisa na Mratibu wa Lishe kwa Kinamama, Watoto na Vijana kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Tufingene Malambugi, anasema mjamzito anayenyonyesha anashauriwa kupewa vyakula mchanganyiko vinavyomtosha.

Anashauri umuhimu wa jamii kutambua na kuzingatia lishe bora kwa mjamzito, akifafanua: "Hii itamuwezesha mama kujenga afya bora katika mwili wake na mtoto, kutoa maziwa ya kutosha kwa ajili ya mtoto wake pia kuweza kuhudumia familia yake."

Malambugi anasema mjamzito na anyonyeshae, wote wanapaswa kuzingatia milo mitatu inayojitosheleza kila siku, pia vitafunwa au milo midogo muda wa kati mara mbili kwa siku.

Hata hivyo, anafafanua kwa mama anayenyonyesha, anahitaji milo mingi midogo na akifafanua: "Mama ale vyakula vya mchanganyiko vinavyopatikana kwa urahisi. Mama ale mboga za majani na matunda kwenye kila mlo, matunda yenye rangi ya njano na mboga za majani yana virutubisho zaidi."

Malambugi anashauri mlo mwingine unaopaswa kuepukwa iwezekanavyo, ni kunywa chai au kahawa na milo inayofanana nayo, lengo ni kuzuia kufyonzwa mwilini madini ya chuma, hali inayochangia upungufu wa damu.

"Ni vyema kunywa chai au kahawa saa moja kabla au moja baada ya kula, kunywa maji yaliyochemshwa ya kutosha kila siku angalau (glasi nane au lita moja na nusu), mama apate muda wa kupumzika angalau dakika 30 kila siku wakati wa mchana.

"Mama aepuke kunywa pombe na kuvuta sigara wakati wa ujauzito na wakati wa kunyonyesha, mama mjamzito aepuke kula vitu ambavyo si chakula kama vile udongo, mkaa au chaki ambavyo vinaweza kuleta madhara katika mwili," anaelimisha.

"Mama anayenyonyesha, aepuke kupika mboga za majani kwa muda mrefu ili kuzuia upotevu wa virutubishi," anaendelea

Malambugi anakumhusha haja ya kila wakati wa kuandaa chakula kuendane na haja ya kunawa mikono kwa sabuni na maji safi yanayotiririka.

"Weka vyombo na sehemu ya kutayarishia chakula katika hali ya usafi, pika nyama, samaki na mayai mpaka viive kabisa ili kuepuka maambukizi.

"Osha mboga mboga kabla ya kuzikata, kisha zipikwe mara moja kwa muda mfupi na kuliwa mara moja kwa muda mfupi, ili kupata virutubishi. Osha vizuri matunda na mboga mboga zinazoliwa,"anasema.

### UPANGAJI MLO

Malambugi anasema mjamzito au anayenyonyesha anapaswa kupata milo mitatu kamili na vitafunwa walau mara mbili kwa siku, zikiwamo viazi, mihogo na ndizi mbichi na magimbi

Pia, anaorodhesha nafaka kama vile mahindi, mtama, mchele, ulezi na ngano, sambamba na nyama, maharage, njegere, karanga, mbaazi, fiwi na dengu.

"Vyenye asili ya wanyama ni kama vile nyama za aina zote, mayai, maziwa, samaki, dagaa, ndege aina ya kuku, bata, njiwa na wadudu wanaoliwa kama vile senene na kumbikumbi. Vyakula hivi vina utomwili au protini kwa wingi kwa ajili ya kujenga mwili,"anasema.

Mtaalamu huyo anataja matunda kama embe, ndizi mbivu, papai, pera, chungwa, ubuyu, nanasi, pesheni parachichi na zambarau, ubuyu, ukwaju na matunda ya asili, yana vitamin inayolinda mwili na kusaidia ufanyaji wake kazi katika mifumo mbalimbali.

Pia, anataja mboga za majani kama vile mchicha, majani ya maboga, kisamvu, matembele, bamia yana madini na Vitamini yanayosaidia kulinda mwili usishambuliwe na magonjwa, ikiasadiana na lishe kama karoti, nyanya chungu, matango, mlenda, boga na biringanya.

Mengine katika orodha hiyo inajumuisha sukari na mafuta, ambayo yanapoongezwa kwenye mboga zingine huboresha ufyonzaji wa baadhi ya vitamin, hali kadhalika nguvu mwilini.

### FAIDA ZILIZOPO

Mlo wa mafuta yanatajwa kuongeza uzito usiopungua kilo 12 kwa mlaji wakati wa ujauzito kila mwezi, inazuia upungufu wa damu na kuboresha ukuaji mtoto kimwili na kiakili. Anafafanua: "Mahitaji ya chakula na virutubishi ni makubwa mama anaponyonyesha kuliko wakati wa ujauzito."

Lishe bora, pia ina manufaa ya kupunguza uwezekano wa kupata mtoto mwenye uzito pungufu, kujifungua kabla ya wakati au kupata mtoto mfu.

"Mahitaji ya chakula na virutubishi huongezeka katika kipindi cha ujauzito, kwa ajili ya mtoto aliye tumboni na mama mwenyewe. Lishe bora wakati wa ujauzito husaidia ukuaji mzuri wa mtoto aliye tumboni na kuutayarisha mwili wa mama kwa ajili ya kunyonyesha," anasema.

Maatalamu huyo anainisha upungufu wa damu, unavyochangia kupunguza uwezekano wa mama kuzaa mtoto mwenye uzito pungufu na akajifungua kabla ya wakati au hata kupata mtoto mfu, haki inapokuwa mbaya zaidi.

### KAULI YA MUHUSIKA

Mkazi wa Chinyambwa, Sara Mazengo, anasema akina mama wengi hasa wajawazito na wanaonyonyesha wamekuwa wakila vitu ambavyo havina virutubisho kwa watoto.

Anashauri wataalamu lishe kutoa elimu ya kila mara, hali itakayochangia kinamama kunyonyesha watoto kwa kufuata maelekezo ya wataalam kupitia maziwa ya mama na si kuwapa vitu vingine.

"Unajua kinachosababisha mama anampa mtoto uji au maziwa ya ng'ombe kabla ya kutimiza miezi sita ni kutokana na kwamba anaona mtoto hashibi kutokana na wepesi wa maziwa na huu unatokana na vyakula ambavyo anakula. Sasa hii elimu ya vyakula ni muhimu, maana ukuaji mtoto unachangiwa na vitu vingi," anasema.



Mlo maalum kwa mnyonyeshaji. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



# Wauguzi, wakunga hatarini kufutwa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAUGUZI na wakunga nchini ambao watakuwa hawajahuisha leseni zao ndani ya miezi sita watachukuliwa hatua ikiwamo kufutwa kwenye daftari la uuguzi na ukunga.

Iwapo uamuzi huo utafikiwa, wataalamu hao hawataruhusiwa kutoa huduma kwenye vituo vya afya vya umma au binafsi.

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga, Agnes Mtawa, alisema juzi kwenye kikao kazi cha kuwajengea uwezo wa kusimamia maadili na utendaji kazi wauguzi wakuu wa wilaya kinachoendelea jijini hapa.

"Nitoe rai kwa wauguzi na wakunga ambao hawajahuisha leseni zao ndani ya miezi sita. Sheria inamtaka msajili awafute katika daftari na kama watafutwa, hawatakuwa na sifa ya uuguzi na ukunga," alisema Mtawa.

Msajili huyo alisema hadi sasa ni asilimia 75 ya wauguzi na wakunga wameshahuisha leseni zao na asilimia 25 waliobaki bado wanaendelea kuwaangalia kwenye kanzidata yao kwa kuwa wapo wauguzi ambao wamefariki dunia, kustaafu na wengine wamebadilisha kada.

Alisema kwa wale ambao bado wanatoa huduma za uuguzi na ukunga wanakumbushwa kuwa na leseni kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga Na. 1 ya mwaka 2010 na kwa wale watakaoshindwa, sheria inasema hawaruhusiwi kuendelea kutoa huduma ya uuguzi na ukunga. "Taarifa imeshapelekwa kwa wahusika na orodha imetayarishwa kwa wale waliohuisha na wale ambao hawajahuisha watakuwa wamejifuta na hawatokuwa na sifa ya kuendelea kutoa huduma za afya na waajiri wao watatakiwa kuwachukulia hatua za kuwafuta kazi kwenye vituo vya umma na vile vya binafsi," alisisitiza.

Mtawa aliwakumbusha wauguzi kuzingatia maadili kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria kwa kuwa kumekuwa na malalamiko ya hapa na pale kuhusu utoaji wa huduma kwenye vituo vya afya.

Naye Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Kalidushi Charles, alisema malalamiko mengi yanaelekezwa kwa wauguzi kwa kuwa sehemu kubwa wanakaa na wagonjwa kwa muda mrefu na ndio watu wa kwanza kupokea wagonjwa, hivyo wanapaswa kusimamia sheria.

"Tunafahamu sasa hivi serikali imeboresha miundombinu, kumekuwa na vituo vingi vya kutolea huduma za afya ambavyo vinafanya upasuaji kwa hiyo vituo hivi havitakuwa na maana kama sisi wasimamizi wa hizo huduma hatutasimamia vizuri ili wananchi wapate huduma kama azma yake Rais," alisema.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Wakuu wa Wauguzi ambaye ni Muuguzi Kiongozi kutoka Wilaya ya Bukombe, Fadhiri Meshack, alisema mafunzo hayo yanawajengea uwezo viongozi kwa ajili ya kupanua wigo wa uelewa ili kuwasimamia na kuwasaidia wauguzi wanaowaongoza.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, akiangalia papai lenye uzito wa kilo tano, alipotembelea maonyesho ya wakulima Nanenane, katika viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma juzi. Kushoto ni mkulima wa zao hilo, Happy Emanuel.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana waonywa kuchagua wala rushwa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KUELEKEA uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu, vijana wametahadharishwa kutofanya makosa watakayojutia kwa miaka mitano ijayo kwa kuwachangua viongozi watoa rushwa. Hayo yalibainishwa jana na Mchungaji wa Huduma ya Holygost Fire International Mirecle Centre, Idda Sirwa, alipokuwa akizungumza na vijana jijini hapa.

Sirwa alisema kuwa vijana wakiwachagua viongozi kwa njia za rushwa itawagharimu, kutokana na fedha walizozipokea.

Alisema kuna hatari ya kuwapata viongozi watakaongoza nchi kwa maslahi yao binafsi kutokana na fedha na vitu mbalimbali walivyotoa kwa ajili ya kutaka kuchaguliwa. "Hivyo ninawasihi vijana kote nchini kuhakikisha kwenye uchaguzi huu wa mwaka huu, kujiepusha na kutokubali kundanganyika kwa rushwa kwani hali hiyo itawagharimu," alisema. Naye Mchungaji wa Kanisa la TAG Mnadani jijini Dodoma, Marcel Mushi, aliwataka vijana kujikita kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji ili kujiinua kiuchumi.

Alisema pamoja na kujihusisha na huduma mbalimbali za kiroho na kijamii, watumike pia kwenye uzalishaji ili wajikwamue na umaskini. Naye Samweli Mwandoboka aliwataka vijana waliojiandikisha kwenye daftari la wapigakura katika uchaguzi wa mwaka huu kutumia haki yao ya msingi kwa kujitokeza kupiga kura na kuwachagua viongozi wenye maadili na hofu ya Mungu.

Pia aliwataka vijana hao kutojihusisha na vitendo viovu, badala yake wajihusishe na ubunifu wa miradi huku wakimtumikia Mungu ili wafanikiwe.

# Kaya 7,900 kuhakikiwa

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

KAYA 7,936 wilayani Kondoa zilizokuwamo kwenye kipindi cha kwanza cha mpango wa kunusuru kaya masikini awamu ya tatu chini ya Mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF), zinafanyiwa uhakiki ili kubaini kaya hewa na zile zenye wanufaika wasio na sifa.

Uhakiki huo ni sehemu ya utekelezaji agizo la Rais John Magufuli, alilolitoa mapema mwaka huu alipokuwa akizindua kipindi cha pili cha TASAF awamu ya tatu.

Rais Magufuli aliagiza kabla ya shughuli zozote za kipindi cha pili kuanza, uhakiki wa walengwa ufanyike nchini kote ili kuondoa kaya zote ambazo zimepoteza sifa.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mratibu wa Tasaf Wilaya ya Kondoa, Donald Jidai, wakati wa mafunzo kwa wawezeshaji kuhusu uhakiki wa walengwa, alisema kaya hizo ni kutoka katika vijiji 63.

Jidai alisema uhakiki huo utatumia teknolojia ya kisasa ambayo itasaidia kupatikana kwa walengwa wenye sifa ambao wanastahili kuendelea na mpango huo katika kipindi cha pili kinachotarajia kuanza hivi karibuni.

"Uhakiki huu tutatumia vishkwambi ambavyo vitatusaidia kupata taarifa sahihi na kubaini walengwa wa kweli. Lakini pia kwa wale ambao watakuwa wamehitimu, wataondolewa kwenye mpango kupisha wengine kwani tayari wameshapata uwezo wa kujikimu na familia zao," alisema.

Pia alisema pamoja na kutumia mfumo wa kisasa kufanya uhakiki, wawezeshaji wamelishwa viapo ili kutenda haki katika mchakato wote wa uhakiki. Alisema vigezo vinavyotumika kuwaondoa wanufaika katika mpango huo ni pamoja na mtu kuwa kiongozi wa chama au serikali pia mstaafu katika utumishi.

"Mnufaika aliyekufa ataondolewa kwenye mpango kama alikuwa peke yake bila wategemezi. Lakini kwa yule ambaye alikuwa mkuu wa kaya na amekufa basi atachaguliwa mwingine ili kuwa mwakilishi wa kaya maskini," alisema.

Aidha Ofisa kutoka TASAF Makao Makuu, Deo Shakiula, alisema ili kutekeleza agizo la Rais Magufuli na pia kuondoa dhana iliyojengeka kwa jamii ya kuwemo walengwa hewa, wataanza utekelezaji kwa kusafisha daftari.

"Mafunzo ambayo yanafanyika yanalenga kujenga uelewa wa pamoja wa namna zoezi hili la uhakiki wa walengwa likavyofanyika" alisema Shakiula.





# Waiomba serikali kudhibiti wanaojenga kwenye mikondo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wananchi wameiomba serikali kuwazuia wenzao wanaojenga makazi kwenye mikondo ya maji kwa kuwa wanahatarisha maisha yao hasa kipindi cha mvua zinazosababisha mafuriko.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wakazi wa mtaa wa Songambele, Kata ya Utengule–Usongwe ambao baadhi ya nyumba zao zimebomoka na wengine kuzingirwa na maji kutokana na maji kukosa uelekeo baada ya baadhi ya wenzao kuyazuia.

Mmoja wa wananchi hao, Chibili Mtafya, alisema katika eneo hilo hawajawahi kushuhudia mafuriko, lakini mwaka huu yamewakumba baada ya mvua kubwa kunyesha kwa muda wa siku mbili mfululizo.

Alisema walilazimika kuwapatia hifadhi wenzao ambao nyumba zao zilibomoka na kwamba chanzo ni maji kukosa uelekeo baada ya nyumba mpya kujengwa kwenye mkondo mkuu wa maji.

"Ni kweli mwaka huu kumekuwa na mvua nyingi, lakini haikuwa sababu ya mafuriko kuja kwenye maeneo yetu haya, kuna wenzetu wamejenga huko Songambele na wamezuia maji ndio yakaja huku kwetu," alisema Mtafya.

Alisema baada ya kuingia kwenye makazi yao walikubaliana na kutengeneza mfereji ambao waliuelekeza barabarani ili yasiwadhuru na kwa sasa barabara hiyo haipitiki kwa gari wala pikipiki.

Aliwaomba viongozi wa serikali za mitaa kuepuka kuruhusu watu kuuziana maeneo ya mikondo ya maji kwa maelezo kuwa hali hiyo inawaathiri hata wasiohusika kutokana na tamaa ya wachache.

Naye Sifumwike Msyani, alisema mafuriko yamesababisha uharibifu kwenye mazao hasa maharage ambayo yameanza kuungua kutokana na maji kuzidi.

Alisema wanaogopa kupiga dawa ya ukungu kutokana na mashamba kubadilika na kuwa chepechepe.

# TMDA kudhibiti uingizaji bidhaa zisizosajiliwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imeahidi kufanya msako wa kudhibiti na kuzuia uingizwaji pamoja na uuzaji wa bidhaa zisizosajiliwa na mamlaka hiyo na kuweka ulinzi kwenye njia za panya katika mikoa ya Songwe, Rukwa na Mbeya.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Nyanda za Juu kusini, Anita Mshighati, wakati akizungumza na Nipashe, kuwa miongoni mwa sababu zinazochangia uuzaji wa bidhaa ambazo hazijathibitishwa na mamlaka yao ni uwapo wa njia za panya kwenye mikoa hiyo ambayo wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu hupitisha vifaa tiba na dawa. Alisema baada ya kubaini uingizwaji holela wa dawa na vifaa tiba, mamlaka hiyo imeanzisha operesheni ya kukagua na kuangalia bidhaa zinazopitishwa kwenye mipaka pamoja na kudhibiti njia za panya kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya.

"Nchi yetu ni kubwa kuna mipaka ambayo siyo rasmi watu wasio waaminifu hutumia njia hizo kupitisha bidhaa ambazo hazina ubora wowote, maeneo kama Songwe na Rukwa, inapatikana na nchi jirani hivyo mwingiliano ni mkubwa bidhaa nyingi zinauzwa huko hivyo katika kudhibiti hilo tumekuwa tukishirikiana na halmashauri," alisema Mshighati.

Alisema moja ya majukumu ya mamlaka hiyo ni kutoa vibali vya kuingiza na kutoa bidhaa ambazo ni dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambazo zimethibitishwa na mamlaka zote ikiwamo ya TMDA.

Pia alisema bado wananchi hawana taarifa ya kutosha kuhusu mamlaka hiyo kuhama kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), kwa kuwa bado wanaendelea kutoa taarifa za masuala ya vyakula vinavyotiliwa shaka.

Aliwahamasisha kutumia dawa kulingana na maelekezo ya wataalamu wanayopewa ili wasiweze kupata madhara kwa kuhakikisha wanaangalia muda wa matumizi kuisha kabla ya kutumia.

Aliwakumbusha wananchi kutoa taarifa wanapobaini uingizwaji holela wa dawa pamoja na taarifa kwa yeyote anayepata madhara baada ya kutumia dawa.

Mkazi wa Kigoe wilayani Mbarali, Bahati John, alisema maonyesho ya Nanenane yamempa fursa ya kujifunza masuala mbalimbali ikiwamo elimu juu ya dawa na vifaa tiba, huku akisema kikubwa ni kukagua na kuangalia muda wa matumizi ya dawa hizo.




Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, akionyesha sampuli za dawa na vifaa tiba, ambavyo vinaruhusiwa na mamlaka hiyo, kutumika katika maonyesho ya wakulima Nanenane katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# H'shauri zatakiwa kuanzisha magulio kulinda wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAIMU Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA), mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Malanga, amezishauri halmashauri za wilaya katika mikoa hiyo, kuanzisha magulio ya pamoja mahususi kwa ajili ya kuuza mazao kwa kutumia mizani ambayo imekidhi vigezo lengo likiwa ni kuondokana na matumizi ya ndoo na ndonya ambazo zinamuibia mkulima.

Malanga alitoa wito huo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu utoaji elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya vipimo vilivyothibitishwa na wakala huyo.

Alisema ili kudhibiti wimbi la matumizi ya ndoo na ndonya katika kuuza na kununua mazao ni vyema sasa halmashauri za wilaya katika mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini zikaanzisha magulio ya pamoja ambayo yatakuwa ni kitovu cha uuzaji na ununuzi kwa kuwa na mizani rasmi.

Alisema njia hiyo itamsaidia mkulima kupata faida baada ya kuuza mazao yake kuliko ilivyo sasa wafanyabiashara ndio wanufaika zaidi.

"Maeneo ya vijijini ndiko kuna shida kubwa ya matumizi ya ndoo na ndonya, hawatumii kabisa mizani kuuza mazao yao, na wafanyabiashara wanapenda kweli kwa sababu wanapata faida, nazishauri halmashauri kutenga masoko maalumu ya uuzaji mazao na kuweka mizani ambayo itatumiwa katika uuzaji na ununuzi," alisema Malanga.

Alisema Wakala wa Vipimo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini utaanza operesheni ya kukagua bucha zote za nyama kuangalia utekelezaji wa agizo la kuhakikisha mizani zote zimepigwa chapa na wakala huyo.

Alisema bucha itakayobainika mizani yake haina chapa, itatozwa faini pamoja na kuchukuliwa hatua nyingine za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Aliwakumbusha wananchi kutokubali kuuziwa nyama au kitoweo chochote katika bucha bila kupimwa kwenye mizani iliyothibitishwa na wakala wa vipimo na wanapobaini kuwa hawajafuata maagizo hayo watoe taarifa mara moja.





# Dk. Shein apigia chapuo sekta ya kilimo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, amesema bila maendeleo endelevu yenye tija katika sekta ya kilimo, amani na utulivu uliopo utatetereka kwa sababu ya kudhoofika kwa sekta hiyo na kuathiri hali ya uhakika wa chakula.

Dk. Shein aliyasema hayo juzi katika ufunguzi wa Maonyesho ya Nanenane yaliyofanyika Langoni, Wilaya ya Magharibi 'A' Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Dk. Shein alisema uhakika wa chakula unapoathirika mifumko ya bei huibuka kwa kile chakula kidogo kilichopo, hivyo watakuwapo watakaomudu na watakaoshindwa kukabiliana na mifumko hiyo.

Alisema malalamiko, bugudha, hasira na chuki zitakuwa haziishi kwa kuwa njaa inazaa athari nyingi mbali ya hizo za kisaikolojia, hata za kiafya, pia subira na uvumilivu, hupotea mambo ambayo yanaweza kusababisha utendaji wa maovu mbalimbali na kuvunjika kwa amani na utulivu.

Alisema ukosefu wa amani na utulivu hauzuii jitihada za maendeleo zisifanikiwe bali unateketeza mpaka yale maendeleo ambayo yalikwishafikiwa kama ambavyo nzige wanavyoteketeza mazao shambani.

"Mwenyezi Mungu atuepushie mbali nchini mwetu na awaondoshee wenzetu waliofikwa na balaa hilo la kukosa amani na utulivu," alisema Dk. Shein.

Alisema Serikali ya Zanzibar kwa kuzingatia umuhimu wa uhakika wa chakula na lishe na uimarishaji wa kilimo endelevu, imekuwa ikitekeleza kwa vitendo Sheria Namba 5 ya mwaka 2011 ya uhakika wa chakula na lishe, Zanzibar.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021, serikali imeongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 88.17 ya mwaka 2019/2020 hadi kufikia Sh. bilioni 129.86 kwa mwaka 2020/2021.

Alisema serikali imelipa kipaumbele suala la uchumi wa bahari na sasa umekuwa ni miongoni mwa vyanzo vikubwa ya kukuza uchumi hasa kwa nchi za bahari kuu zikiwamo za visiwa.

Alisema serikali imelifufua Shirika la Uvuvi la Zanzibar (ZAFICO), ili liweze kuimarisha shughuli za uvuvi na kuleta mageuzi ya uvuvi nchini ikiwamo mkazo katika uvuvi wa bahari kuu ambao una tija zaidi.

Kwa upande wa sekta ya mifugo, Rais Dk. Shein alisema, serikali inaendeleza sekta hiyo kwa hatua kadhaa ikiwamo kutoa elimu kwa wafugaji, huduma za chanjo na tiba kwa wanyama, imenunua mtambo wa kutengenezea chakula cha kuku na samaki pamoja na kuwasomesha vijana 45 udaktari wa wanyama.

Pia Dk. Shein alisema kwa upande wa sekta ya uvuvi, mipango ya baadaye ni kuanza ujenzi wa diko (sehemu ya mnada) na soko la kisasa la samaki katika eneo la Malindi litakalotoa huduma kwa wananchi wapatao 6,500 na ujenzi wa soko hilo umeshaanza kutokana na msaada wa Sh. bilioni 18 kutoka Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mariam Abdalla Sadalla, alisema kaulimbiu ya maonyesho hayo mwaka huu ni "Tudumishe amani ni na utulivu kwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini".

Alisema kilele cha maonyesho hayo ni Agosti 8 na taasisi 219 zimeshiriki na kupita idadi ya mwaka jana ya 172 huku akizisisitiza zilizopewa maeneo ya kudumu kuyajenga ili kuepusha gharama za ujenzi zinazofanywa na wizara yake kila yananapofika maonyesho.

Katika ufunguzi huo, Pia Rais Dk. Shein alitembelea mabanda ya maonyesho pamoja na kujionea vifaa mbali mbali vya uvuvi, kilimo na ufugaji na kupata maelezo ikiwa ni pamoja na kuyazindua matreka mapya 20.

# Viongozi CCM watakiwa kuzingatia maadili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

Mjumbe wa Kamati ya siasa ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman, amewataka viongozi wa CCM kufanya kazi kwa maslahi ya chama na kuzingatia sheria na maadili ya chama hicho.

Alisema viongozi wa chama hicho ni vyema wakakumbuka maadali ya chama chao ikiwa ni wakati wa uchaguzi na baada ya kumalizika kwa uchaguzi.

Aliyasema hayo wakati alipokua akizungumza na wajumbe wa mkutano mkuu wa wazazi Mkoa wa Kusini Pemba mwishoni mwa wiki.

Alisema matokeo yanayotolewa baada ya uchaguzi si kwamba mgombea ameshinda wakati kamati za maadili zinaendelea na vikao vyake kwa umakini na kuzingatia kanuni, sheria na misingi ya Chama cha Mapinduzi.

"Katika uchaguzi wetu tutahakikisha tunawapata wagombea halali kura zitapigwa kihalali, kwa uwazi na kuhesabiwa kila mgombea atapata kwa mujibu wa kura ambazo zitapigwa na wajumbe," alisema.

Aliwataka wagombea hao kuwa na hekima na busara ili kuhakikisha kila mmoja anapata haki yake.

Alisema matokeo sahihi ni yanayotolewa baada ya uchaguzi na sio yanayotangazwa kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya watu.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Kusini Pemba, Mohamed Ali Khalfan, aliwataka wajumbe kuchagua viongozi wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi.

Aliwataka wagombea ambao kura zao hazikutosha kuwa wavumilivu na kushirikiana na wezao bila kuvunjika moyo ili kukiletea ushindi chama cha CCM katika uchaguzi mkuu mwaka huu.



Balozi mdogo wa China Zanzibar, Xie Xiaowu (wa pili kulia), akikabidhi msaada wa dawa na vifaa tiba kwa Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, uliotolewa na Serikali ya China, katika hafla iliyofanyika Bohari Kuu ya Dawa Maruhubi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# China yatoa msaada wa dawa, vifaa vya mil. 5/-

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR imepokea msaada wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni miatano kutoka Serikali ya Watu wa China wenye lengo la kuimarisha huduma za afya nchini.

Balozi mdogo wa China, Zanzibar, Xie Xaiowu, alikabidhi msaada huo kwa Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, katika hafla iliyofanyika Bohari Kuu ya Dawa, Maruhubi.

Balozi Xie alisema msaada huo wenye dawa za magonjwa tofauti na vifaa tiba vikiwamo vya kujilinda na maradhi ya corona ni kielelezo cha uhusiano mzuri kati ya wananchi wa China na Zanzibar.

Alisema China itaendelea kusaidia Zanzibar katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii ikiwamo ya afya ili iweze kupiga hatua ya maendeleo kwa urahisi.

Aliwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kufuata maagizo ya viongozi na wataalamu wa afya wakati wa kipindi cha corona na kusaidia kupunguza kasi ya maambukizi na hatimaye kuyadhibiti.

Akipokea msaada huo, Waziri Hamad, aliishukuru Serikali ya China kwa misaada yake inayotoa kwa Zanzibar hasa katika kuimarisha huduma za afya.

Alisema wakati Zanzibar ilipopata maradhi ya corona, China ilikuwa nchi ya kwanza kutoa vifaa na wataalamu waliosaidia katika kupambana na maradhi hayo.

Waziri Hamad alisema baadhi ya dawa alizopokea zinahitajika kwa kiasi kikubwa wakati huu hasa katika wodi za wazazi na za wagonjwa wa figo.

Alisema dawa na vifaa tiba hivyo vitasambazwa katika hospitali kuu ya Mnazimmoja, hospitali za wilaya na vituo vyote vya afya Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi wa kuwahudumia wananchi.

Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa, Zahran Ali Hamad, alisema msaada wa dawa na vifaa tiba vilivyotolewa zitaongeza ufanisi katika sehemu ya upasuaji na zitasaidia kupoteza damu nyingi wananchi watakaopatwa na ajali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**ZARIA AHMAD RASHIDI** amepotelewa na Cheti cha elimu ya chuo (TRANSCRIPT) alichosomea katika chuo cha SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE, Alichomaliza mwaka 2019. Na chenye namba ya mtihani: **AGC.668845**
Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Taarifa ya polisi; **MOR/MOR/RB/577603/202**

115845402

## KUPOTEA KWA KADI

**HABIBU EPHRON MWAKIGWE.** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **MITSUBISHI - ERF.** chassis **99051** yenye namba za usajili no.**T397 BZU** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi Polisi Taarifa: **DAR/BUG/RB/578455/2020**

115846102

## KUPOTEA KWA KADI

**JOASH MBONEA KAVUTA.** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **Toyota - Allion** yenye namba za usajili no. **T859 DAV.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MBA/RB/580712/2020**

115846002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZINIA**

**KUITWA SHAURINI (SUMMONS).**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**

**WILAYA YA KAHAMA**

**SHAURI LA MADAI NO.102/2020**

**MADAI HALMASHAURI YA MJI KAHAMA DHIDI MDAIWA KIKUNDI CHA MAPINDUZI (NYIHOGO)**

1. **Rehema Makula(Mwenyekiti wa kikundi)**
2. **Sitta S. Katekela(Katibu wa kikundi)**

Kwa kuwa imelazimika uhudhurie ili kuja kujibu madai ya pesa Tsh.11,814,000/=unazodaiwa na halmashauri ya mji,unaamriwa na Jamuhuri uhudhurie mbele ya mahakama siku ya jumatatu tarehe 07/08/2020 saa 2:00 asubuhi na ukifika usiondoke bila ruhusa ya mahakama

Unaonywa kwamba ikiwa utakataa kupokea wito huu au kupuuza bila udhuru wa maana hati itatolewa kukulazimisha kuhudhuria na utashtakiwa kwa kosa hilo.

Hati hii imetolewa kwa AMRI yangu na MUHURI wa mahakama hii leo Jumatano Tarehe 01/07/2020

Sahihi ya hakimu PRIMARY COURT MAGISTRATE KAHAMA

115845902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:49..2020**

**Mdai: MARIA PIUS**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: VICENT JOSEPH MSHANGA**

**Ombi la Mdai: MARIA PIUS**

**Kwa: VICENT JOSEPH MSHANGA WA MADUKA KUMI.**

**Madai ya: TALAKA, MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO WATATU.**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 11 mwezi 08 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 08 mwezi 07 mwaka 2020.

115845502

## CHETI KIMEPOTEA



**Edward Fidel** amepotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index No. S0654/0085** cha Rwambaizi Sekondari, alihitimu mwaka 2013. Amepotelewa pia cheti cha kidato cha sita chenye **index No. S0115/0650** cha shule ya Sekondari Kahororo, alihitimu mwaka 2016. Vyeti hivyo viliibwa, ametoa taarifa polisi na kupewa Na. **KAG/BUK/RB/143011/2020** na **KAG/BUK/RB/142559/2020.**
Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa polisi au apige simu Na. **0758-632226**

115845002

## KUPOTEA KWA KADI

**Shoki Ibrahim M. Pishoki** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya Usajili namba **T375 BJQ** aina ya **TREKTA** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **PWA/BAG/RB/574019/2020**

115845102

## KUPOTEA KWA KADI

**Theobard Peter Katinda** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya Usajili namba **T191 DJK** aina ya **TOWNACE NOAH** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KBA/RB/2260/2020**

115845202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI** **FORM II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 81/2020**

**Ombi la GODFREY ROBERT kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu RAYMOND ROBERT**
**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnano tarehe 14/8/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Sahihi ya Hakimu PRINCIPAL PRIMARY COURT URBAN DODOMA

115845702

## KUPOTEA KWA KADI

**Robert Renatus Magoso** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya Usajili namba **T274 DKL** aina ya **IST** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KW/RB/3981/2020**

115845302


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

# Jamhuri yashinda rufani makosa yasiyo na dhamana kudhaminiwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania, imekubali rufani dhidi ya Jamhuri kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wa kuruhusu makosa yasiyo na dhamana yaruhusiwe kudhamiwa kwa kuwa kifungu kinachozuia dhamana hakikinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uamuzi huo ulisomwa jana baada ya jopo la majaji watano liliketi katika mahakama hiyo, likiongozwa na Stella Mugasha, Gerald Ndika, Jacobs Mwambegele, Mwanaisha Kwariko na Ignas Kitusi.

Akisoma uamuzi huo, Naibu Msajili, Eva Nkya, alisema kifungu namba 148(5) A mpaka E havikinzani na Katiba na vinakidhi masharti.

"Kifungu hicho kinaelezea kwamba makosa ambayo hayadhaminiki na kinakidhi matakwa ya kikatiba, mahakama hii inatamka kwamba uamuzi wa Mahakama Kuu umebatilishwa" lilisema jopo hilo.

Mapema mahakama hiyo ilikubali hoja za Jamhuri katika rufani iliyokatwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) wakipinga uamuzi wa Mahakama Kuu ulioruhusu dhamana kwa baadhi ya makosa ya jinai yasiyokuwa na dhamana.

Makosa yaliyoko katika kifungu hicho ni pamoja na mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha, uhaini, ugaidi, kutakatisha fedha na kesi za dawa za kulevya.

Mengine ni mtuhumiwa aliyewahi kufungwa miaka 30 jela hataweza kupata dhamana, mtu aliyepewa dhamana akashindwa kutekeleza masharti ya dhamana au akaruka dhamana, pale ambapo mtu anatakiwa kukaa ndani kwa ajili ya usalama wake, pale ambapo kosa linazidi Sh. milioni 10.

DPP na AG walikata rufani hiyo wakipinga uamuzi wa Mahakama Kuu katika wa kesi iliyofunguliwa na Dickson Sanga akitaka makosa hayo yawe na dhamana kwa sababu kifungu kilichokuwa kinazuia kinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uamuzi huo wa Mahakama Kuu ulitolewa na jopo la majaji watatu, likiongozwa na Mwenyekiti wake, Benhajj Masoud, Seif Kulita na Juliana Masabo Mei 18, mwaka huu kwamba Kifungu cha 148 (5) cha Sheria ya Makosa ya Jinai kinakiuka Katiba.

Katika rufani yake DPP na AG walidai kifungu hicho hakikiuki Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Walidai kwamba Mahakama Kuu ilikosea kisheria kutamka kuwa kifungu namba 148(5) kinakiuka Ibara ya 13(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia, mahakama hiyo ilifanya makosa ya kisheria kutamka kuwa Kifungu hicho Namba 148 cha Sheria ya Makosa ya Jinai hakithibitishwi na Ibara ya 15(1) na (2)(a ) ya Katiba wa Jamhuri ya Muungano, kwamba kifungu hicho kilikiuka Katiba pamoja na kwamba mjibu rufani alishindwa kuthibitisha madai yake pasi kuacha shaka.

Hoja nyingine ya warufani hao ni kwamba, Mahakama Kuu ilikosea kupinga kifungu hicho bila kuzingatia shida zinazoweza kusababishwa katika mfumo mzima wa utawala wa haki za jinai nchini.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (kushoto), akiambatana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Gerald Kusaya (wa pili kushoto) walipotembelea Jukwaa la Watafiti na Wachambuzi wa Sera kwenye Maonyesho ya Wakulima Nanenane, Mkoa wa Simiyu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wasisitizwa utamaduni mahudhurio ya kliniki

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WAJAWAZITO mkoani Shinyanga wametakiwa kujenga utamaduni wa kuhudhuria kliniki mapema ili kupata huduma na ushauri wa afya.

Aidha, wakifanya hivyo itasaidia kuwaepusha kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Mganga mfawidhi wa Hospitali ya Kolandoto Manispaa ya Shinyanga, Zephania Msunza, alibainisha hayo kwa gazeti hili kuhusu hali ya vifo vitokanavyo na uzazi.

Alisema moja ya sababu kubwa ya vifo vitokanavyo na uzazi ni wajawazito kutohudhuria kliniki kwa wakati na kusubiri nyakati za mwisho na wengine wameshafariki.

"Natoa wito kwa wajawazito mkoani Shinyanga, wajenge utamaduni wa kuhudhulia kliniki mapema, ili wapate vipimo pamoja na ushauri wa kutunza ujauzito na siku ya kujifungua wajifungue salama na kupunguza vifo vya uzazi," alisema Msunza.

"Takwimu za vifo vya watoto wachanga kwa mwaka jana kuanzia Januari hadi Machi vilitokea vifo tisa, lakini mwaka huu kwa kipindi hicho hicho wamefariki watano na kupunguza vifo vinne," aliongeza.

Naye Mratibu elimu huduma ya afya ya uzazi mkoani Shinyanga, Halima Hamisi, alisema kuanzia Januari hadi Machi mwaka jana kulikuwa na vifo 16, huku mwaka huu vikiwa 11.

Kwa upande wa vifo vya wajawazito kwa kipindi hicho vilikuwa 12, mwaka huu 11, na kwamba elimu itawasaidia wananchi wengi kujitambua.

# Jafo: Zaidi ya tril. 3/- zimejenga miundombinu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amesema katika kipindi cha miaka mitano Sh. trilioni 3.463 zimetumika kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Jafo alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumzia mafanikio katika sekta ya miundombinu ikiwa ni siku ya tatu ya maadhimisho ya Siku ya TAMISEMI.

Alisema hatua hiyo imesaidia kuongezeka kwa mtandano wa barabara za lami kwa mamlaka hizo kutoka kilomita 1,325.49 mwaka 2015 hadi kufikia kilomita 2,024.99 mwaka 2020.

"Fedha hizi zilizotumika ni pamoja na Sh. trilioni 1.03 ambazo zilizoelekezwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na Sh. trililioni 1.98 ambazo ni fedha maalumu zilizotumika kujenga mtandao wa barabara za lami katika miji ya kimkakati, manispaa na halmashauri za miji na Jiji la Dar es Salaam.

Alisema kwa upande wa barabara za changarawe kwa mamlaka hizo kulikuwa na barabara zenye urefu wa kilomita 22,089 na baada ya maboresho zimefikia urefu wa kilomita 24,193 ikiwa na ongezeko kwa asilimia 11, huku serikali ikiimarisha barabara za vumbi (udongo) na kufikia urefu wa kilomita 82,428, wakati madaraja makubwa yaliyojengwa ni 99.

Alisema mtandao wa barabara zenye hali nzuri na wastani umeongezeka kutoka kilomita 61,798.45 hadi kufikia kilomita 63,164.74 sawa na ongezeko la barabara zenye hali nzuri na wastani urefu wa kilomita 1,366.29.

"Hii inafanya barabara zenye hali nzuri kutoka asilimia 56 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 58 mwaka huu, inaonyesha utashi wa Rais wa kuhakikisha wananchi wanatengenezewa mtandao wa barabara na hii imesaidia hata wakulima kusafirisha mazao yao, siku za nyuma watu walikuwa wanateseka sana, tunamshukuru Rais kwa kuwezesha hili," alisema.

Waziri Jafo alisema mbali na barabara, lakini serikali imejenga stendi za kisasa 24, stendi za malori, masoko ya kisasa za mamlaka ya serikali, madampo ya kisasa katika baadhi ya miji.

Kuhusu mradi wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam (DART), Jafo alisema ikiwa kazi za awamu ya pili ya mradi huo ikishika kasi, awamu ya kwanza imekuwa na mafanikio ya kuongeza abiria kutoka 75,000 kwa siku hadi kufikia abiria zaidi ya 200,000 kwa siku.

"Bado tunaendelea na maandalizi ya kumtafuta mtoa huduma wa kudumu atakayekuwa na uwezo kutoa huduma ya mabasi 305 ikilinganishwa na mtoa huduma wa sasa ambaye ana uwezo wa kutoa huduma ya mabasi 140,"alisema.

Naye Meneja wa Mfuko wa Barabara, Eliud Nyauhenga, alisema magari kuzidisha mzigo ni moja ya changamoto inayorudisha nyuma juhudi za serikali katika maendeleo ya sekta ya barabara.

Alisema uzidishaji mizigo kwenye magari ni kinyume na matakwa ya sheria na imekuwa ikichangia uharibifu mkubwa wa barabara.

"Kwa mfano kwa sasa huko vijijini magari yanayokwenda kubeba mazao yamekuwa yakizidisha uzito jambo ambalo linaharibu miundombinu," alisema.



# TORRES

## AMRITHI SANE MAN CITY

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City imemsajili winga anayekuja juu, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 20 kutoka Valencia.

Stats Perform News inaelewa kwamba, mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya Hispania chini ya umri wa miaka 21, amewagharimu City pauni milioni 21.1.

City walikuwa wakihusishwa na mawinga kadhaa baada ya kuondoka kwa Leroy Sane aliyetua Bayern Munich ambaye alithibitishwa mwanzoni mwa Julai, huku Torres akitajwa kusaini mkataba wa miaka mitano kukaa hapo kwenye dimba la Etihad.

City inayonolewa na Pep Guardiola ambaye sasa anaonekana ataendelea kubaki na klabu hiyo kwa msimu mwingine, imemsajili Torres na kuzipiku Barcelona, Juventus na Liverpool, ambazo zilikuwa zimetuma ofa.

"Nina furaha kubwa kujiunga na City," alisema Torres. "Kila mchezaji anataka kujiunga na timu ya ushambuliaji bora kama Manchester City ambayo ni moja kati ya timu zenye washambuliaji bora duniani.

"Pep alinishawishi, hasa kwa staili yake ya kucheza soka la kuvitia na kwa utulivu, kitu ambacho nakipenda, na yeye ni kocha ambaye anapenda timu inayoshambulia. Kuwa naye hapa ni ndoto iliyotimia."

Torres anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji vijana wa Hispania wenye kiwango cha kuvutia zaidi na atakuwa na mafanikio makubwa zaidi hapo baadaye, akiwa ameanza kuichezea Valencia akiwa na umri wa miaka 17 mwaka 2017 na msimu wa 2018-19 alifunga mabao 24 kwenye LaLiga.

# CONTE AHUBIRI UMOJA MILAN

**MILAN, Italia ward**

KOCHA Mkuu wa Inter Milan, Antonio Conte amehubiri umoja wakati uvumi ukienea kuhusu majaliwa yake wakati akikodolea macho mafanikio kwenye Ligi ya Europa.

Majaliwa ya Conte yametawala vyombo vya vya habari tangu alipoishutumu klabu hiyo kutoa ulinzi mdogo kwake yeye na wachezaji baada ya kumaliza mchezo wa mwisho wa Serie A msimu huu wa ushindi wa 2-0 dhidi ya Atalanta.

**Inter imeripotiwa kwamba ina iangalia kwa makini nafasi ya Conte baada ya kudumu hapo kwa msimu mmoja, huku kocha wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri na kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino wakihusishwa na kuchukua mikoba yake pale Nerazzurri.**

Lakini kuelekea mchezo wa jana Jumatano wa Ligi ya Europa hatua ya mtoano wa timu 16 dhidi ya Getafe, Conte aliwaambia waandishi wa habari: "Ninapozungumza ni kwa ajili ya Inter.

"Sio muhimu sana kwangu, ni muhimu zaidi kwa Inter. Kama ilivyo mara zote ninapoulizwa. Tujaribu kuzungumza kuhusu sisi, kitu ambacho kinatuweka sisi karibu kwa pamoja chini ya mwavuli mmoja."

Inter ilimaliza msimu wa Serie A 2019-20 katika nafasi ya pili nyuma ya Juve baada ya kupata pointi 82 kutoka mechi 38 ikifiisha pointi sawa na walizozipata msimu wa 2009-10 chini ya Jose Mourinho wakati wakishinda mataji matatu.

Na sasa miamba hao wa Italia wameelekeza nguvu zao kuhakikisha wanatwaa taji la Ligi ya Europa.

# CASEMIRO: KUIVAA CITY BILA MASHABIKI FAIDA KWA MADRID



**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa Real Madrid, Casemiro amesema kucheza wakati milango imefungwa bila mashabiki pale kwa Manchester City inaweza kuwasaidia mabingwa hao wa La-Liga kupindua matokeo.

Madrid imesafiri kwenda Etihad kwa ajili ya mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora dhidi ya vijana hao wa Pep Guardiola, mchezo utakaopigwa Ijumaa hii, huku mchezo wa kwanza wakiwa wamepoteza 2-1.

Gabriel Jesus na Kevin De Bruyne ndio walikuwa wauaji kule mjini Madrid – ambapo nahodha wao Sergio Ramos alitolewa nje kwa kadi nyekundu.

Madrid ina mlima mkubwa wa kuupanda mjini Manchester, lakini nyota Casemiro anaamini kikosi hicho cha kocha Zinedine Zidane kinaweza kunufaika kwa kucheza bila mashabiki.

"Bila mashabiki ni mchezo tofauti kabisa," alisema Casemiro mchezaji wa kimataifa wa Brazil akiiambia Esporte Interactivo.

"Utakuwa mchezo mzuri sana na mgumu kwa timu zote mbili, lakini sisi ni Real Madrid na tunajua tuna nafasi ya kusonga mbele.

"Hawatakuwa na mashabiki wao na hilo litatupa ahuweni kwetu sisi. Lakini wachezaji ni wale wale, kocha ni yuleyule na wote tunajua kwamba mchezo utakuwa mgumu."



# NEYMAR

## AFURAHIA UBORA WAKE PSG

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR anaamini sasa anafurahia kiwango chake bora zaidi tangu alipojiunga na mabigwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain.

Baada ya kuwasili kutoka Barcelona kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 mwaka 2017, Neymar sasa ameshinda mataji tisa na kufunga mabao 74 katika mechi 85 alizocheza kwenye mashindano yote.

Neymar ambaye amekuwa akihusishwa mara kwa mara kurudi kwa miamba wa LaLiga, Barca tayari ameshasherehekea mafanikio ya kubeba ubingwa wa Ligue 1, Coupe de France, Coupe de la Ligue na Trophee kwa msimu unaoisha wa 2019-20 wakati PSG sasa macho yao yakiwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Miaka hii mitatu imekuja na ujuzi mwingi. Nimeishi nyakati za furaha na wakati mwingine nyakati ngumu, hasa wakati niliposhindwa kulipwa kwa sababu ya majeraha," alisema Neymar, ambaye yeye na PSG wanajiandaa kwenye mchezo wao wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta, akinukuliwa na tovuti ya timu hiyo.

"Huku wachezaji wenzangu wananisaidia, niliweza kuyashinda hayo na sasa tunachoangalia zaidi ni kuhusu kiwango cha timu yetu dimbani ili kutwaa mataji.

"Mashabiki wetu, klabu na kila shabiki wa timu yetu anatakiwa kutuunga mkono kwa sasa katika mchezo wowote.

"Naamini kwamba leo naishi katika nyakati bora zaidi hapa jijini Paris. Tumetengeneza familia kwa malengo makubwa kwa ajili yetu.

"Tunataka kumaliza msimu huu kwa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Tunapigania hilo, kwa sababu hatujawahi kuwa karibu nalo."

Msimu wa 2019-20, Neymar amefunga mabao 13 kwenye Ligue 1 na19 katika mashindano yote kwa kikosi hicho cha Thomas Tuchel.

## BUNDESLIGA: MARUFUKU BIA, MASHABIKI WA TIMU NGENI

**MUNICH, Ujerumani**

SOKA la Ujerumani linakabiliwa na kupoteza utamaduni wake, kama mashabiki wataruhusiwa kuingia viwanjani msimu ujao wa Ligi Kuu ya Bundesliga.

Kwani hawataruhusiwa mashabiki wa timu inayocheza ugenini kusimama uwanjani na pia utamaduni wa kunywa bia hautakuwapo uwanjani.

Chama cha Klabu za Soka za Ligi ya Ujerumani (DFL), kilifanya mkutano Jumanne kwa ajili ya kuweka masharti hayo, ikiwa ni sehemu ya kujikinga na mlipuko wa virusi vya corona.

Klabu za Bundesliga zitaweza kuruhusu mashabiki uwanjani kama tu masharti hayo yatazingatiwa, baada ya kumaliza msimu wa 2019-20 bila mashabiki uwanjani.

Katika taarifa yake, ligi hiyo imesema wamekubaliana na klabu za Bundesliga kwamba hawatauza tiketi kwa mashabiki wa timu itakayokuwa inacheza ugenini hadi mwishoni mwa mwaka huu.

Pia DFL ilisema klabu zimekubaliana masharti ya mashabiki kutosimama kwenye mechi.

Kunywa bia wakati wa mechi ni utamaduni maarufu kwa soka la Ujerumani, lakini haitaruhusi msimu ukianza hadi Oktoba 31 na kwamba baada ya hapo wataangalia kama wataweza kuruhusu tena.

Msimu mpya wa Ligi Kuu ya Ujerumani utaanza Septemba 18, mwaka huu.

## SOLSKJAER ADOKEZA KUMRUDISHA SMALLING

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amedokeza kwamba, Chris Smalling anaweza kubakia Manchester United kwa siku zijazo baada ya kumaliza msimu kwa kiwango cha kuvutia akiwa anacheza kwa mkopo kule Roma.

Mlinzi Smalling Jumanne alisema anajisikia vibaya kwamba hatacheza tena msimu mwingine kwa Roma.

Mlinzi huyo wa kati alikuwa nguzo imara kwa kikosi hicho kwa msimu huu uliomalizika nchini Italia, lakini sasa mkataba wake wa mkopo umemalizika kule katika mchezo wake wa mwisho dhidi ya Juventus Jumamosi iliyopita.

Aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter kuhusu kuondoka Roma: "Nimehudhunishwa kwamba siwezi kumaliza kile nilichokianza msimu huu.

"Mapenzi niliyoonyeshwa kwa muda mfupi, kwa kweli sitasahau.

"Nataka kuwashukuru na kuwatakia kila la heri wachezaji wakielekea kwenye mchezo wao wa Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla."

Solskjaer amebainisha kwamba, nyota huyo wa zamani wa Fulham anaweza kuwa sehemu ya kikosi chake pale Old Trafford msimu ujao.

"Nafikiri Chris ameonyesha kuwa ni mchezaji mwenye thamani kubwa na naamini ataendelea kuwa hapa Manchester United," alisema Solskjaer. Smalling amecheza mechi 30 kwa Roma katika Serie A na wamemaliza nafasi ya tano kwenye msimamo, huku akiwa ameanza mechi tano kwenye Ligi ya Europa.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DYBALA AMFUNIKA RONALDO SERIE A

**Nyota wa Juve wapata mafanikio zaidi huku Szczesny akitajwa kipa bora na De Vrij akitwaa...**

**TURIN, Italia**

PAULO Dybala ametajwa kuwa mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi kwenye Serie A (MVP) kwa msimu wa 2019-20, baada ya kuwa kiungo muhimu wakati Juventus ikitetea taji la Ligi Kuu, lakini Cristiano Ronaldo amekosekana kwenye orodha ya tuzo hizo.

Dybala alifunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho sita kwenye ligi kwa 'Bianconeri' hao ambao walitwaa taji la Italia kwa mara ya tisa mfululizo.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina ameshinda tuzo hiyo kwa sababu ya kiwango binafsi na kujitoa kwenye timu, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Stats Perform.

Takwimu hizo zilichukuliwa kutoka kwenye mechi za mashindano ya Coppa Italia, Supercoppa Italiana na Serie A.

Ronaldo alifunga mabao 31 kwa Juve, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ureno alizidiwa na mshambuliaji Ciro Immobile, ambaye aliifikia rekodi ya Gonzalo Higuain ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja, akitikisa nyavu mara 36 kwa Lazio.

Kulikuwa na mafanikio zaidi kwa Juventus katika tuzo hizo, ambapo golikipa wake, Wojciech Szczesny akitajwa kipa bora, huku mlinzi wa Inter, Stefan de Vrij akitwaa tuzo ya beki bora.

Alejandro Gomez alizawadiwa kwa kuwasaidia Atalanta kumaliza katika nafasi ya tatu kwa mara ya pili mfululizo, huku Dejan Kulusevski alitajwa mchezaji bora kijana wa msimu baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia kule Parma anakocheza kwa mkopo.

Kulusevski mwenye umri wa miaka 20 raia wa Sweden, alisajiliwa na Juventus kutoka Atalanta katika dirisha la Januari na akapelekwa Parma kucheza kwa mkopo kwa kipindi cha msimu kilichobakia.

## KWA UFUPI

**GREALISH KUBAKI VILLA**
NAHODHA wa Aston Villa, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 24, atapewa mkataba mpya wa kulipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki, baada ya Manchester United kuonyesha haina nia ya kutaka kumsajili. ***(Sun)***

**CITY, ROBERTO BADO**
KLABU ya Manchester City bado haijawasiliana na Barcelona kuhusu beki wa kulia Sergi Roberto mwenye umri wa miaka 28, licha ya kuhusishwa kwa kiasi kikubwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania. ***(Manchester Evening News)***

**LIVER YAJITOSA KWA LEWIS**
LIVERPOOL ipo tayari kulipa dau la pauni milioni 10 kwa beki wa kushoto wa Norwich na Ireland Kaskazini, Jamal Lewis mwenye umri wa miaka 22, wakati inatafuta nani wa kuvaa viatu vya Andy Robertson. ***(Daily Mirror)***

**HOJBJERG KUTUA SPURS**
KIUNGO wa kati wa Southampton raia wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 24, anatarajia kujiunga na Tottenham kwa pauni milioni 15, huku beki wa Uingereza, Kyle Walker-Peters mwenye umri wa miaka 23, akipata mkataba wa kudumu wa pauni milioni 12. ***(Telegraph)***

**ISMAILA AGOMBEWA EPL**
LIVERPOOL, Crystal Palace na Wolves zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili winga wa Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 22, kutoka Watford iliyoshushwa daraja. ***(Watford Observer)***

**LEICESTER YAIGUSA BARCA**
KLABU ya Leicester City imefanya mazungumzo na Barcelona kuulizia ikiwa inaweza kumchukua mshambuliaji wa Ureno, Francisco Trincao mwenye umri wa miaka 20, kwa misimu miwili ya mkopo, huku kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja kwa pauni milioni 45. ***(Guardian)***

**EVERTON YAMPOTEZEA EVERTON**
EVERTON haitamsajili nyota mwenye jina sawa na klabu hiyo, Everton kwa kuwa mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 24, ameonekana kuwa tayari kujiunga na Benfica ya Ureno kutoka Gremio. ***(Goal)***

**IVANOVIC KUMFUATA ANCELOTTI**
ALIYEKUWA beki wa kulia wa Chelsea, Branislav Ivanovic amesema kuna uwezekano akawasiliana na aliyekuwa kocha wake, Carlo Ancelotti anayeinoa Everton. ***(Sun)***

**SOUTHAMPTON KWA ZEEFUIK**
KLABU ya Southampton imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa Groningen, Deyovaisio Zeefuik mwenye umri wa miaka 22, lakini raia huyo wa Uholanzi anaaminika anapendelea kuhamia Ligi Kuu ya Ujerumani. ***(Southern Daily Echo)***

**EZE AWINDWA PALACE**
MSHAMBULIAJI wa Queens Park Rangers, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 22, anawaniwa na mahasimu wao wa jiji la London, Crystal Palace na West Ham, huku klabu hiyo inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, ikiweka thamani ya mchezaji huyo kuwa ni pauni milioni 20. ***(Evening Standard)***

**NEWCASTLE JICHO KWA KING**
KLABU ya Newcastle inammezea mate mshambuliaji wa Bournemouth raia wa Norway, Josh King mwenye umri wa miaka 28, na kiungo wa kati wa Wales, David Brooks, 23. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

# YONDANI, YANGA SC BADO HAKIELEWEKI

**Na Faustine Feliciane**

DAU la usajili limetajwa kuwa chanzo cha kuchelewa kufikiwa muafaka kati ya Yanga na beki kisiki wa klabu hiyo, Kelvin Yondani aliyemaliza mkataba wake msimu huu.

Juzi beki huyo alikutana na uongozi wa klabu yake kwa ajili ya mazungumzo ya kuongeza mkataba, lakini hata hivyo mazungumzo hayo yalivunjika bila kufikia muafaka.


Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi wa klabu hiyo, Dominick Albinius, amesema licha ya mazungumzo hayo kutofikiwa muafaka, bado pande hizo zinaendelea na mazungumzo kuhakikisha nahodha huyo wa zamani anasaini mkataba mpya.

"Jana (juzi) kila upande ulikuwa na matakwa yake, tumejadiliana, lakini hatukufikia mwisho, ila haimaanishi kuwa tumeshindwana hapana, mazungumzo yanaendelea kama ilivyo kwa Juma Abdul," alisema Albinius.

Hata hivyo, taarifa za ndani kutoka klabu hiyo, zinaeleza kuwa Yondani amegoma kusaini mkataba mpya baada ya kupewa mapendekezo ya klabu ambayo yanamtaka kusaini mkataba mpya bila fedha za usajili na kubaki mshahara wa kila mwezi.

Inadaiwa pande hizo mbili zitakutana tena kujaribu kuangalia namna ya kumaliza suala hilo la usajili wa beki huyo ambaye aliwahi kuichezea Simba.

PAMOJA SANA...




Mshambuliaji wa Aston Villa ya England na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta (katikati) akiwa na wachezaji wa klabu yake ya zamani ya Simba, viungo Mkongo Deogratius Kanda (kushoto) waliyewahi kucheza naye TP Mazembe ya DR Congo na Mzambia Clatous Chama, walipokutana jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Kocha Prisons ajiweka sokoni

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Tanzania Prisons, Adolph Rishard amesema, yupo huru kuitumikia klabu yoyote itakayojitokeza kuhitaji huduma yake na kumpa maslahi makubwa ukilinganisha na aliyokuwa anayapata katika klabu yake hiyo, ambayo amemaliza nayo mkataba.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, kocha huyo alisema endapo watafikia makubaliano ambayo yanaendelea na timu yake hiyo, hana budi kubaki lakini ikijitokeza ofa nono hawezi kuiacha.

"Sasa hivi mimi nipo huru, mkataba wangu tayari umemalizika kama kuna timu yoyote ambayo itanipa maslahi makubwa zaidi ya niliyokuwa nayapata katika timu hii, nitakuwa tayari kuondoka na kwenda kuanza maisha mengine," alisema Rishard, ambaye amefanikiwa kuibakiza Prisons Ligi Kuu Bara baada ya kumaliza katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo msimu huu zimeshuhudiwa timu nne zikishuka daraja moja kwa moja huku ya tano ikifuata baada ya kushindwa kufuzu kupitia mechi ya mchujo dhidi ya timu ya Daraja la Kwanza.

Aidha, alisema kama ataendelea na timu hiyo, atahakikisha anaunda kikosi ambacho kitaleta ushindani katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao utaanza rasmi Septemba 6, mwaka huu, katika viwanja mbalimbali hapa nchini.

"Kama tukikubaliana, nitafanya mabadiliko makubwa kwa sababu wachezaji ambao mpaka sasa sihitaji kuendelea nao tayari nimeandika majina yao katika ripoti yangu ambayo tayari nimeikabidhi pamoja na wale ambao nitawaongeza kwa ajili ya kuongeza nguvu kikosi changu," alisema.

Nipashe lilipomtafuta Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Adamu Kifukwe, alisema bado wanaendelea kufanya mazungumzo na kocha huyo ambaye amepambana kuhakikisha timu hiyo inapata mafanikio.

Alisema wana matumaini makubwa ya kuendelea na kocha huyo kwa kile anachodai kuwa ameipigania timu hiyo kwa kiasi kikubwa mpaka kuifikisha hapo ilipo, kwa kufanikiwa kubakia Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha timu yao inaanza maandalizi mapema ya kujiandaa na msimu ujao kwa lengo likiwa ni kujenga kikosi imara ambacho kitaonyesha ushindani mkubwa.

"Malengo yetu ni kuhakikisha tunashika nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa ni pamoja na kuanza kambi mapema ili wachezaji wazidi kuiweka sawa miili yao vile vile wachezaji waweze kuzoeana kabla ligi kuanza," alisema katibu huyo.

Singida United, Ndanda FC, Lipuli FC na Alliance ni timu zilizoshuka daraja moja kwa moja msimu huu huku Mbao FC nayo ikishuka baada ya kushindwa kufurukuta dhidi ya Ihelfu FC ya Mbarali, Mbeya kwenye mechi za mchujo.

## Mayanga aachiwa rungu la usajili Ruvu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ruvu Shooting imesema haikurupuki kwenye usajili au kuangalia timu fulani inasajili sana, badala yake itasajili kwa matakwa ya benchi lao la ufundi chini ya Kocha Mkuu, Salum Mayanga na si vinginevyo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo Masau Bwire alisema jana kuwa wao kama Ruvu Shooting hakuna eneo ambalo hawaliheshimu kama la usajili, ambalo halitakiwi kufanyiwa utani au kujaribu wachezaji.

Masau alisema hayo alipokuwa akielezea mustakabali wa klabu hiyo baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

"Eneo ambalo halitakiwi kufanyiwa utani ni eneo la usajili, kwa sababu ukikosea tu basi utalia msimu mzima. Kwa hiyo tuko makini katika hili na tutasajili kwa kufuata maelekezo ya mwalimu kwa sababu yeye ndiye anajua kikosi chake kilikuwaje, kibadilike vipi na nani asajiliwe, nani atoke," alisema msemaji huyo wa Ruvu Shooting na kuongeza.

"Kikosi kizuri cha soka kinaimarishwa na usajili mzuri, sisi hatukurupuki, au kuangalia fulani amefanya nini. Lakini kama kuna mchezaji atataka kuondoka sisi hatumzuii kwa sababu vijana maisha yao ni mpira, akiona anahitajika sehemu nyingine sisi huwa hatuna kinyongo ingawa jinsi wachezaji wetu wanavyolelewa na kuthaminiwa, sidhani kama wanaweza kukubali kuondoka haraka haraka hivi." alisema.

Kuhusu kocha Mayanga, Bwire amesema kuwa kocha huyo ameonyesha dhamira ya kubaki na timu hiyo, lakini uongozi wa Ruvu Shooting pia umeonyesha nia ya kumbakisha.

## Mtifuano Daraja la Kwanza Znz leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inatarajiwa kuendelea leo, Alhamisi kwa kupigwa michezo minne katika viwanja vya Mau Kisiwani Unguja.

Majira ya saa nane mchana itapigwa michezo miwili ambapo katika Uwanja wa Mau A, Miembeni City itavaana na Mwembe Makumbi City wakati huo huo katika Uwanja wa Mau B kutakuwa Black Sailor itamenyana na Kikwajuni.

Majira ya saa 10:000 alasiri, itapigwa michezo miwili katika Uwanja wa Mau B, Mundu itavaana na Dulla Boys, wakati katika Uwanja wa Mau A, Idumu itakuwa na kibarua pevu dhidi ya Bweleo.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha wa Kikwajuni, Salim Husun, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kidogo kwa upande wao kutokana na wachezaji kukaa muda mrefu bila ya kufanya mazoezi ya pamoja.

"Kuwarejesha wachezaji mchezoni kutakuwa na ugumu kidogo katika mechi hizi za mwanzo kwa kuwa walikaa takribani miezi minne bila ya kucheza ligi, hivyo ni wajibu viongozi kufanya juhudi ili tuhakikishe timu zinafanya vizuri," alisema.

# Michezo

Alhamisi Agosti 6, 2020

Nipashe





Dybala amfunika Ronaldo Serie A

HABARI UK 22

SINTOFAHAMU...




Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck (kulia), akiwa na wasaidizi wake, Selemani Matola na Kipa wa Makipa Mwarami Mohammed (katikati) katika moja ya mazoezi ya timu hiyo, kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena uliopo Bunju, jijini Dar es Salaam. Sven amemaliza mkataba na klabu hiyo na haijafahamika kama ataongezwa ama la. **PICHA: SIMBA**

# SVEN AONDOKA, SIMBA WAGAWANYIKA MARA 2

●●● Sababu za kumtimua zawaumiza, wachezaji wapewa wiki moja, Bodi ya Wakurugenzi sasa kuamua...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukamilisha majukumu yake kwa kuibebesha Simba mataji mawili, lile la Ligi Kuu Bara na Kombe la FA, hatimaye Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mbelgiji Sven Vandenbroeck ameondoka zake na kurejea kwao Ubelgiji huku akiacha uongozi wa timu hiyo ukiwa umegawanyika mara mbili kuhusu hatima yake.

Sven ambaye mkataba wake umemalizika mwishoni mwa msimu huu, ameondoka juzi na kurejea kwao kwa mapumziko huku akiwa hajui mustakabali wa maisha yake ya baadaye ndani ya klabu hiyo kama ataongezwa mkataba ama la.

Lakini taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jana kutoka chanzo chetu ndani ya Simba, uongozi wa klabu hiyo umegawanyika mara mbili kuhusu suala la kumpa mkataba mpya, huku baadhi ya wajumbe walioketi wiki hii wakitaka aendelee kuinoa Simba na wengine wakipendekeza waachane naye.

Chanzo hicho, kilieleza hadi sasa kocha huyo amekuwa akiuumiza vichwa uongozi wa klabu hiyo na kuwafanya wagawanyike mara mbili ambapo wanaotaka aongezwe mkataba wana hoja nzito wakiegemea katika mafanikio aliyoyapata msimu huu kwa kutwaa makombe mawili, huku wanaopinga wakidai kwamba alikuwa na matatizo na baadhi ya wachezaji.

"Ni kweli Sven alikuwa na matatizo yake ambayo kila binadamu anayo, ila suala hili la kuondoka au kubaki ndilo limeleta sintofahamu, huku uongozi ukitafakari vigezo ambavyo wanaweza kumuacha ilhali ameweka rekodi nzuri katika timu yetu kwa kutwaa mataji mawili chini ya uongozi wake," kilieleza chanzo chetu bila kupepesa macho.

Kilisema kitendo cha kufanya vizuri na kutwaa mataji mawili huku timu ikicheza vizuri, kimewaweka mtegoni viongozi hao na kuwafanya watafakari mara mbili kuhusu kumwongeza mkataba au kuachana naye na kuleta mwingine.

"Muda uliobakia ni mfupi sana ukizingatia wachezaji wamepewa mapumziko ya wiki moja, kwa hali hii mchakato wa kupata kocha mwingine na timu kuanza naye maandalizi ya msimu mpya, kwa muda huo ni mdogo sana ila bado tunasubiri maamuzi ya Bodi ya Wakurugezi," kilifafanua.

Alipotafutwa Katibu wa timu hiyo, Arnold Kashembe, alisema masuala ya kocha na benchi la ufundi yapo chini ya Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, hivyo kwa sasa wanachokifanya ni kusajili wachezaji wachache ambao wamependekezwa katika ripoti ya benchi la ufundi.

"Tumemaliza msimu tukiwa tumebeba mataji matatu, Ligi Kuu, Kombe la FA na Ngao ya Jamii, mawili yakiwa chini ya kocha wetu Sven, suala la kurejea lipo katika bodi na sasa tutasajili wachezaji ambao watasaidia timu yetu kufanya vizuri kwa msimu unaokuja ili kutetea mataji yetu," alisema katibu huyo huku akifafanua kuwa wiki hii watageukia usajili wa wachezaji wa kimataifa.

Tayari Simba imekamilisha usajili wa wachezaji watatu wa ndani ambao ni beki wa kulia kutoka Lipuli FC, Kameta Duchu, mshambuliaji kutoka KMC, Charles Ilanfya na beki wa kati, Ibrahim Ame kutoka Coastal Union aliyesajiliwa juzi usiku kwa mkataba wa miaka miwili.

## AZAM FC: SURE BOY ANAITAKA YANGA SC

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Klabu ya Azam imekubali yaishe kwa kuamua kuiita Yanga mezani kuzungumza dili la kumsajili kiungo wao, Abubakari Salim 'Sure Boy', baada ya mchezaji huyo kuwaeleza dhamira yake ya kutaka kuondoka kwenda kujiunga na timu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Awali, uongozi wa Azam FC ulieleza kupokea barua kutoka Yanga ikieleza nia yao ya kuomba kufanya mazungumzo ya kumsajili Sure Boy, lakini miamba hiyo ya Chamazi, Mbagala jijini Dar es Salaam ikakataa, kabla ya jana kuridhia na kukaribisha ofa.

"Yanga walifuata utaratibu kwa kuleta barua ya kuomba kumsajili, lakini kocha mkuu (Aristica Cioaba) alisema kiungo huyo yupo kwenye mipango yake na tulipomuuliza Sure Boy alisema hana mpango wa kuondoka, ndipo tukawajibu Yanga mchezaji huyo hauzwi," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' na kuongeza.

"Lakini jana usiku (juzi usiku), nilizungumza tena na Sure Boy naye akaniambia anataka kuondoka, hivyo tunaisubiri Yanga ije tena maana awali walipoleta barua yao tuliwaambia hauzwi."

Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa zilizofikia Nipashe jana muda mfupi kabla ya kwenda mitamboni, zieleza Yanga ilitarajia kupeleka ofa yao kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo anayeelezwa kuvutiwa sana na timu hiyo tangu utotoni.

Mapema jana alipoulizwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi wa Yanga, Dominick Albinius, kuhusu usajili wa Sure Boy, alisema kila kitu wanakifanya kwa kufuata utaratibu na kama suala hilo lipo, likikamilika litawekwa hadharani.

Yanga inataka kuziba nafasi hiyo ya kiungo mkabaji baada ya kuachana na nahodha wao Papy Tshishimbi waliyeshindwa kukubaliana katika suala la usajili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >